TOLEO LA 04

ISSN 2961 - 6255

# USAFIRI ARDHINI



## MHE. RAIS DKT. HUSSEIN ALI MWINYI ATEMBELEA JENGO LA LATRA

Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi............ UK. 5

## MHE. DKT. MPANGO, MHE. SILLO WAKABIDHI TUZO ZA LATRA KWA WASAFIRISHAJI BORA UK. 1

Julai - Septemba 2024



**CPA HABIBU JUMA SULUO**
*Mkurugenzi Mkuu - LATRA*

# TAHARIRI

Nakukaribisha tena katika toleo la nne la jarida la USAFIRI ARDHINI kutoka Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) lililokusanya taarifa mbalimbali za Mamlaka kuanzia mwezi Julai hadi Septemba, 2024. Lengo ni kukuhabarisha wewe msomaji na mdau wetu kuhusu masuala yanayogusa sekta ya Usafiri Ardhini Nchini.

Miongoni mwa mambo makubwa tunayojivunia katika kipindi hiki ni kufanikiwa kutoa tuzo kwa wasafirishaji Bora na Salama kwa mabasi ya njia ndefu ambapo Mhe. Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, na Mhe. Daniel Baran Sillo (Mb), Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi na Mwenyekiti wa Baraza la Taifa la Usalama Barabarani, Agosti 26, 2024 walikabidhi tuzo hizo katika sherehe za ufuguzi wa Maadhimisho ya Wiki ya Nenda kwa Usalama Barabarani yaliyofanyika kitaifa uwanja wa Jamhuri jijini Dodoma. Tuzo hizo zilitolewa kwa makundi matatu ya wasafirishaji ambao ni, wasafirishaji wa kubwa, wasafirishaji wa kati na wasafirishaji wadogo, hakika jambo hili ni mafanikio kwetu kwasababu tumeweza kuwatambuawasafirishaji waliotekeleza kikamilifu masharti ya leseni za usafirishaji.

Vilevile ndani ya jarida hili maridhawa utasoma Makala maalumu inayoakisi mafanikio makubwa ya LATRA mathalan kuongezeka kwa idadi kubwa ya leseni za vyombo vya moto kibiashara zilizotolewa na LATRA katika kipindi cha mwaka 2022/23 hadi 2023/24 na idadi ya leseni za usafirishaji zilizotolewa kila mwaka ziliongezeka kutoka 284,158 hadi 326,576.

Pia tumeendelea kung'ara kupitia ushiriki wetu katika maonesho mbalimbali ikiwemo Maonesho ya 48 ya Kimataifa ya Biashara (Sabasaba) ambapo tuliibuka mshindi wa pili katika kundi la Mamlaka za udhibiti. Pia katika maonesho hayo tulitembelewa na Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, ambaye alijifunza jinsi LATRA inavyotumia mifumo ya TEHAMA katika shughuli zake za kiudhibiti ikiwemo, Mfumo wa Taarifa kwa Abiria PIS unaopatikana kwa anwani ya https://pis.latra.go.tz/ kupitia simu janja au kompyuta.

Hayo ni baadhi tu kati ya mengi utakayosoma kwa kina katika Jarida hili la USAFIRI ARDHINI. Nakusihi usome mstari kwa mstari kufahamu vizuri maendeleo ya sekta ya Usafiri Ardhini na Udhibiti wa huduma za Usafiri Ardhini nchini. Kwa maoni yoyote usisite kuwasiliana nasi kwa namba zetu bila malipo 0800110019 / 0800110020 au kupitia Mfumo wa e- mrejesho unaopatikana kwa anwani https://emrejesho.gov.go.tz/

Nakutakia usomaji mwema
*"Pamoja kwa Usafiri Bora"*

# MHE. DKT. MPANGO, MHE. SILLO WAKABIDHI TUZO ZA LATRA KWA WASAFIRISHAJI BORA



*Mhe. Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania akikabidhi Tuzo ya Mshindi wa Jumla na ya wa kwanza katika kundi la wasafirishaji wakati wenye mabasi 11 hadi 30 kwa TILISHO CO. LTD katika ufunguzi wa wiki ya Nenda kwa Usalama Barabarani uliofanyika uwanja wa Jamhuri jijini Dodoma Agosti 26, 2024.*

Mhe. Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, na Mhe. Daniel Baran Sillo, Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi na Mwenyekiti wa Baraza la Taifa la Usalama Barabarani, Agosti 26, 2024 wamekabidhi tuzo kwa wasafirishaji Bora na Salama kwa mabasi ya njia ndefu katika sherehe za ufunguzi wa Maadhimisho ya Wiki ya Nenda kwa Usalama Barabarani yanayofanyika kitaifa uwanja wa Jamhuri jijini Dodoma.

Tuzo hizo zimetolewa kufuatia shindano la kutafuta Watoa huduma Bora na Salama kwa huduma zilizotolewa Juni, 2023 hadi Julai 2024 kwa makundi ya kwa makundi ya Wasafirishaji Wakubwa, Wakati na Wadogo lililoandaliwa na Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) ikiwa ni sehemu ya kuchochea ushindani wenye ufanisi katika huduma za usafiri wa mabasi.

Akizungumza mbele ya Mhe. Dkt. Mpango, CPA Habibu J. Suluo, Mkurugenzi Mkuu LATRA, amesema Kifungu cha 6(a) cha Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini Sura ya 413, kimeipa LATRA wajibu wa kuhamasisha ushindani wenye ufanisi miongoni mwa watoa huduma zinazodhibitiwa. Ameeleza kuwa, utoaji wa tuzo za Wasafirishaji Bora na Salama, ni sehemu ya utekelezaji wa wajibu huo.

Vilevile amewataja washindi kundi la Wasafirishaji Wakubwa (wenye mabasi zaidi ya 30) kuwa ni, Kampuni ya Shabiby Line mshindi wa kwanza, akifuatiwa na mshindi wa pili kampuni ya Happy Nation na mshindi wa tatu ni kampuni ya ABC Upper Class. Pia CPA Suluo amesema kuwa, kundi la pili (wenye mabasi 11 hadi 30) washindi ni kampuni ya Tilisho ambayo ni mshindi wa kwanza, ikifuatiwa na mshindi wa pili Satco Express na mshindi wa tatu ni Ngasere Co. Ltd.

Ameongeza kuwa, kwa kundi la Wasafirishaji Wadogo (wenye mabasi 3 hadi 10), mshindi kwa kwanza ni Sama Luxury Coach, wa pili ni kampuni ya Achimwene Business na wa tatu ni RATCO Express. Tuzo hizo zimetolewa ili kuchochea matumizi ya mifumo ya utoaji wa huduma bora na salama ya usafirishaji wa abiria kwa ufanisi na ubunifu hususan katika matumizi ya teknolojia.

Aidha, CPA Suluo alifafanua kuwa, mchujo ulifanyika kwa kuzingatia taarifa za mifumo LATRA ya utoaji huduma ambapo wasafirishaji wenye matukio mengi ya ajali, kuchezea Mfumo wa Kufuatilia Mwenendo wa Mabasi, kutoa huduma bila kuwa/kukata bima chini ya viwango stahiki, kusitishiwa leseni za usafirishaji kutokana na kutozingatia Sheria na Kanuni, malalamiko ya

>>>Inaendelea Uk. 02

>>>Inatoka Uk. 01

wateja kuhusu huduma zisizoridhisha, kutowapatia abiria tiketi za kielektroni, upotevu wa mizigo ya abiria, kuzidisha nauli na makosa mengine ya aina hiyo kwa idadi inachofikia 10% ya idadi ya mabasi waliyonayo waliondolewa katika kushindania tuzo hizo.

“Kwa utaratibu huo idadi ya washindani ilipunguzwa hadi kubaki na washindani 15 kwa kila kundi (wakubwa, wa kati na wadogo). Washindani hao 15 kwa kila kundi waliwekwa katika dodoso la kidigitali lilitosambazwa kupitia tovuti ya LATRA na mitandao ya kijamii ili wadau na watumia huduma wawapigie kura, ambapo jumla ya wadau 2,237 walipiga kura kumchagua msafirishaji bora na salama,” alisema.

Akizungumza baada ya kupokea tuzo, Bw. Florence Shirima, muwakilishi wa kampuni ya mabasi ya Tilisho Safaris amesema siri kubwa ya ushindi wao ni kufanya kazi kwa bidii, ubunifu na kutoa huduma bora kwa wateja.

“Tunashukuru kwa ushindi huu tuliopata, kweli tumefarijika sana na tunaahidi kuendelea kuboresha huduma zetu ili mashindano yajayo tuweze kuibuka kidedea, Pia tunawashukuru wateja wetu kwa kutupigia kura kwa wingi na hatimaye kupata ushindi huu mnono, tunawaambia kuwa tuzo hii ni yao,” amesema Bw. Florence.

Kwa upande wake, Bi Stella Nestory, Meneja wa kampuni ya mabasi ya Sama Luxury Coach amewashukuru wadau waliowapigia kura na amesema kuwa tuzo waliyopata imewapa motisha ya kufanya kazi kwa ufanisi na kuongeza kasi ya utoaji wa huduma bora kwa wateja wao na wanaamini watafanya vizuri zaidi mashindano yajayo.

Bw. Priscus Joseph, Katibu Mkuu Chama cha Wamiliki wa Mabasi Tanzania (TABOA) ameipongeza LATRA kwa kutoa tuzo hizo kwa wasafirishaji wa mabasi ya masafa marefu nchini na amesema ni kiashiria tosha cha kuwatambua na kuwathamini wasafirishaji hao na itakuwa chachu kwa wamiliki wa kampuni za mabasi kuongeza juhudi ya kazi na ubora wa huduma.

“Tuzo hizi pia zitaongeza zaidi uhusiano na ushirikiano wetu na LATRA, ni mwanzo mzuri naipongeza sana LATRA na uongozi mzima kwa kufanikisha hili. Pia natoa wito kwa wasafirishaji kutoa huduma nzuri ili waweze kushinda na kupata tuzo,” ameeleza Bw. Priscus.

Kwa upande wake Bw. Ramadhani Msangi, balozi wa usalama barabarani amesema tuzo zilizotolewa zinaonesha jinsi Mamlaka inavyothamini wasafirishaji na lengo ni zuri la kuendelea kuchochea ushindani na kuwahamasisha kutoa huduma bora na salama kwa wateja wao.

Wakati huo huo, Mhe. Sillo amekabidhi vyeti maalum vya utambuzi kwa vyama vya wasafirishaji abiria na mizigo vilivyofanya kazi kwa ushirikiano wa karibu na LATRA hivyo kuiwezesha mamlaka hiyo kutekeleza wajibu wake kwa ufanisi. Vyama vilivyokabidhiwa vyeti vya utambuzi ni Chama cha Wamiliki wa Mabasi Tanzania (TABOA), Chama cha Wamiliki wa Malori Tanzania (TATOA), Chama cha Wamiliki wa Malori Wadogo na Wakati Tanzania (TAMSTOA), Chama cha Wasafirishaji Tanzania (TAT) na Chama cha Wasafirishaji Mizigo kwa Njia ya Barabara Tanzania (TRFA).

>>>Inaendelea Uk. 03

## MHE. DKT. MPANGO, MHE. SILLO WAKABIDHI TUZO ZA LATRA KWA WASAFIRISHAJI BORA



*Mhe. Daniel B. Sillo (Mb), Naibu waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi akitoa cheti cha Utambuzi kwa Chama cha wamiliki wa mabasi Tanzania (TABOA) kwenye ufunguzi wa wiki ya Nenda kwa Usalama Barabarani Uliofanyika uwanja wa Jamhuri jijini Dodoma Agosti 26, 2024.*

>>>Inatoka Uk. 02

## MHE. DKT. MPANGO, MHE. SILLO WAKABIDHI TUZO ZA LATRA KWA WASAFIRISHAJI BORA



*CPA Habibu Suluo, Mkurugenzi Mkuu Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) akiwahudhurisha washindi wa Tuzo za Usafirishaji Bora na Salama kwa mabasi ya njia ndefu kwa Mhe. Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika sherehe za ufunguzi wa Maadhimisho ya Wiki ya Nenda kwa Usalama Barabarani iliyofanyika kitaifa uwanja wa Jamhuri jijini Dodoma Agosti 26, 2024.*

Pia Mhe. Sillo amekabidhi cheti cha utambuzi kwa Chama cha Ushirika na Mikopo cha Watoa Huduma za Bajaji za Abiria na Bodaboda Mkoani Kilimanjaro (KIBABOT SACCOS) kwa kutambua juhudi za cha hicho ambacho ni chama cha kwanza kutoa leseni za LATRA kwa pikipiki za magurudumu mawili na matatu kwa wanachama wao.

> **“Tuzo hizi pia zitaongeza zaidi uhusiano na ushirikiano wetu na LATRA, ni mwanzo mzuri naipongeza sana LATRA .”**
>
> *Bw. PRISCUS JOSEPH*

>>>Inaendelea Uk. 04



## HABARI PICHA




*Mhe. Daniel B. Sillo (Mb), Naibu waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi akitoa Cheti cha Utambuzi kwa Chama cha Ushirika na mikopo cha watoa huduma wa bajaji za abiria na bodaboda mkoani Kilimanjaro (KIBABOT SACCOS) kwenye ufunguzi wa wiki ya Nenda kwa Usalama Barabarani Uliofanyika uwanja wa Jamhuri jijini Dodoma Agosti 26, 2024.*




*CPA Habibu Suluo, Mkurugenzi Mkuu Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA), (wa katikati), Johansen Kahatano, Mkurugenzi Udhibiti Usafiri wa Barabara LATRA (wa pili kulia) na Salum Pazzy, Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano na mawasiliano LATRA (wa kwanza kulia) kwenye picha ya pamoja na wasafirishaji waliowania Tuzo za Usafirishaji Bora na Salama kwa mabasi ya njia ndefu katika sherehe za ufunguzi wa Maadhimisho ya Wiki ya Nenda kwa Usalama Barabarani yaliyofanyika kitaifa uwanja wa Jamhuri jijini Dodoma Agosti 26, 2024.*

# MHE. RAIS DKT. HUSSEIN ALI MWINYI ATEMBELEA JENGO LA LATRA - SABASABA



*Bw. Salum Pazzy, Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) akitoa maelezo kuhusu kazi na majukumu yanayotekelezwa na LATRA kwa Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi wakati alipotembelea jengo la LATRA lililopo viwanja vya Julius Nyerere kwenye Maonesho ya 48 ya Kimataifa ya Biashara (sabasaba) Julai 13, 2024 Jijini Dar es Salaam.*

Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ametembelea jengo la Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) katika viwanja vya Julius Nyerere - Sabasaba kwenye Maonesho ya 48 ya Kimataifa ya Biashara jijini Dar es Salaam Julai 13, 2024 na kushuhudia shughuli za udhibiti zinazotekelezwa na LATRA.

Akitoa maelezo katika jengo la LATRA, Bw. Salum Pazzy, Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano LATRA amesema kuwa, LATRA inatumia Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) katika utoaji wa huduma kwa wadau wake jambo ambalo limesaidia katika kuongeza ufanisi wa shughuli za kiudhibiti.

Aidha, moja ya Mfumo wa TEHAMA alioutaja Bw. Pazzy ni pamoja na Mfumo wa Kufuatilia Mwenendo wa Magari (VTS) unaosaidia kwa kiasi kikubwa kupunguza changamoto za ajali nchini zinazogharimu maisha ya watanzania na mali zao.

Vilevile Bw. Pazzy ameutaja Mfumo mwingine kuwa ni Mfumo wa Taarifa kwa Abiria (PIS) unaomuwezesha abiria kupata taarifa ya basi lilipo, sehemu inayotoka na muda wa kuwasili kituoni na kukagua mwendokasi wa basi alilopanda.

Pia Bw. Pazzy ameeleza kuwa, LATRA na Mamlaka ya Usafiri na Usalama Barabarani Zanzibar (ZARTSA) zinatarajia kuingia mkataba wa makubaliano katika maeneo ya ushirikiano ya masuala ya kiudhibiti kwa kubadilishana uzoefu katika sekta ya usafiri ardhini.

"Mkataba tutakaoingia utaongeza ufanisi katika sekta ya udhibiti kati ya taasisi hizi na haya ni maazimio ya makubaliano baada ya majadiliano yaliyofanyika wakati wa miaka 60 ya Mapinduzi matukufu ya Zanzibar mwezi Januari, 2024" ameeleza Bw. Pazzy.

> **"LATRA inatumia Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) katika utoaji wa huduma kwa wadau wake."**
>
> *Bw. SALUM PAZZY*

# ‘PIS’ YAING’ARISHA LATRA SABASABA

Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) imetengeneza Mfumo wa Taarifa kwa Abiria (Passenger Information System -PIS) unaomuwezesha mwananchi kutambua muda ambao basi la masafa marefu litafika katika stendi ya mabasi aliyoichagua pamoja na kufahamu mwendo wa basi husika pindi akiwa safarini.

Akizungumza baada ya kutembelea Jengo la LATRA kwenye Maonesho ya 48 ya Kimataifa ya Biashara Dar es Salaam (sabasaba), viwanja vya Julius Nyerere na kupatiwa elimu kuhusu mfumo huo, Mhe. Sophia Mwakagenda, Mbunge wa viti maalum Mbeya, ameipongeza LATRA kwa kutumia vizuri Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) katika utekelezaji wa majukumu yao kwa wananchi.

“Nitoe pongezi nyingi kwa LATRA kwa kuja na mfumo huu, nimejifunza vitu vingi hususan maendeleo ya kidigitali kwani naweza kutambua ndugu yangu yuko sehemu gani kwa kuangalia kupitia simu janja yangu na hakuna haja ya kufika stendi na kumsubiri mgeni wako kwa muda mrefu,” ameeleza Mhe. Mwakagenda.

Mhe. Mwakagenda ameongeza kuwa, Mfumo wa PIS unasaidia sana kupunguza mabasi kutembea mwendo hatarishi na unaisaidia LATRA kubaini ratiba walizopatiwa.

Naye CP Awadhi Haji, Mkuu wa Oparesheni na Mafunzo kutoka Jeshi la Polisi Tanzania, ameipongeza Mamlaka kwa ubunifu unaoendana na ukuaji wa teknolojia unaoweza kutatua changamoto mbalimbali za wananchi.

Akizungumza na wadau wa usafiri ardhini waliotembelea jengo la LATRA kwenye Maonesho ya 48 ya Kimataifa ya Biashara (Sabasaba) Dar es Salaam, CPA Habibu Suluo, Mkurugenzi Mkuu wa LATRA amesema Mfumo huo unamuwezesha mwananchi kuwa na taarifa kwa ukaribu zaidi kuhusiana na mwenendo wa mabasi yanayowasili katika vituo mbalimbali nchini.

“Kwa sasa kama una ndugu yako anatoka safari, huna haja ya kumpigia simu kufahamu alipo, bali utaingia kwenye mfumo, cha msingi ufahamu namba ya basi alilopanda. Vivyo hivyo kwa abiria akitumia mfumo huu wa PIS hatokuwa na haja ya kuuliza mahali alipo au muda anaotarajia kufika aendako,” amesema CPA Suluo.

Vilevile ameongeza kuwa, kwa sasa mfumo wa PIS upo katika runinga zilizofungwa kwenye stendi ya mabasi Magufuli Dar es Salaam na stendi ya mabasi nanenane jijini Dodoma,



*Bw. Salum Pazzy, Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) akitoa elimu kuhusiana na Mfumo wa PIS kwa wadau waliotembelea Jengo la LATRA lililopo viwanja vya Julius Nyerere Jijini Dar es Salaam kwenye Maonesho ya 48 ya Kimataifa ya Biashara (sabasaba) Julai 6, 2024.*

>>>Inatoka Uk. 6

# 'PIS' YAING'ARISHA LATRA SABASABA

lakini pia mfumo huo unapatikana kwa anwani ya https://pis.latra.go.tz/ kupitia simu janja au kompyuta, na amewasihi wananchi kutumia mfumo huo utakaowapa taarifa sahihi pindi wawapo safarini au wanapomsubiri msafiri katika stendi mbalimbali za mabasi ya masafa marefu.

Bi. Anna Joseph ni mmoja wa wadau waliotembelea jengo la LATRA katika Maonesho ya 48 ya Kimataifa ya Biashara Dar es Salaam (sabasaba) na amesema kuwa, amefurahishwa sana na mfumo wa PIS ambao unarahisisha muda na kuwapa uhakika wa safari abiria pindi wanapotaka kusafiri, "kwa sasa hata kama sipafahamu ninapokwenda, kupitia mfumo huu wa PIS nitakuwa naangalia vituo mpaka pale nitakapofika safari yangu, pia nimefurahi naweza kuona mwendo wa basi niwapo safarini na nikiona mwendo ni mkubwa nitakuwa namwambia dereva na kondakta wake ili apunguze."

Kwa upande wake, Mha. Eliud Kataraihya, Mkuu wa kitengo cha TEHAMA - LATRA amesema, Mamlaka itaendelea kubuni mifumo



Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
Wizara ya Uchukuzi
Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini
Piga Bure : 0800110019/0800110020

LATRA

MABASI YANAYOWASILI / BUS ARRIVALS
DODOMA

11:46 Jioni
Jumanne, 3 Septemba 2024

| NA. | MMILIKI (OWNER) | NAMBA YA GARI (REG NO) | KUTOKA (FROM) | KWENDA (TO) | KUFIKA (ARRIVALS) | MUDA (TIME) | TAARIFA YA MWISHO (LAST LOCATION) | MUDA WA TAARIFA YA MWISHO (TIME) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | SHABIBY LINE | T116EGM | DAR ES SALAAM | DODOMA | 2024-09-04 | 6:20 Usiku | 5.88 KM N OF MSAMVU ROUND-ABOUT | 11:46 Jioni |
| 2 | IDHA ABDALLAH IDHA (ALLY SAED) | T119DHA | DAR ES SALAAM | DODOMA | 2024-09-04 | 8:27 Usiku | 0.79 KM SE OF MOSEKA | 11:44 Jioni |
| 3 | SHABIBY LINE | T120EGM | DAR ES SALAAM | DODOMA | 2024-09-03 | 5:04 Usiku | 3.68 KM SW OF NANENANE BUS TERMINAL DODOMA | 11:45 Jioni |

mbalimbali itakayomsaidia mwananchi na itakayorahisisha kazi ya udhibiti kwa Mamlaka.

Mfumo huo mpya wa PIS umezinduliwa rasmi kwenye Maonesho ya 48 ya Kimataifa ya Biashara Dar es Salaam (sabasaba) katika viwanja vya Julius Nyerere yanayofanyika kwa siku 16 kuanzia Juni 28 hadi Julai 13, 2024 na katika maonesho hayo, wadau mbalimbali wa usafiri ardhini wameonesha kuvutiwa na kufurahia mfumo huo.

> **"Mamlaka itaendelea kubuni mifumo mbalimbali itakayomsaidia mwananchi na itakayorahisisha kazi ya udhibiti kwa Mamlaka**
>
> *MHA. ELIUD KATARAIHYA*



# CPA SULUO ASHIRIKI MAPOKEZI YA TRENI YA SGR DAR - DODOMA



Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) imeshiriki mapokezi ya safari ya kwanza ya Treni ya Reli ya Kisasa (SGR) iliyoanza safari rasmi kuanzia Dar es Salaam hadi Dodoma. Hatua hii ni sehemu ya utekelezaji wa maelekezo ya Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan Rais, wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ambapo aliagiza safari hiyo kuanza rasmi Julai 25, 2024.

Akizungumza kutokea stesheni ya SGR Dodoma, CPA Habibu Suluo Mkurugenzi Mkuu LATRA amelipongeza Shirika la Reli Tanzania (TRC) kwa juhudi na usimamizi mkubwa wakukamilisha mradi huu na kuanza rasmi safari ya kwanza Dar es Salaam hadi Dodoma chini ya uongozi mahiri wa Mhe. Prof. Makame Mnyaa Mbarawa (Mb) Waziri wa Uchukuzi kwa kufanikisha jambo hili la kihistoria hapa nchini.

Vilevile CPA Suluo ameeleza kuwa, LATRA inajukumu la kudhibiti miundombinu ya Reli pamoja na kuhakikisha kuwa usafiri huu unakuwa rafiki na salama kwa kuboresha sehemu zenye mapungufu ili Wananchi waweze kusafiri salama na kwa wepesi.

“Maafisa wa LATRA wanaendelea kukagua njia ya Dar es Salaam hadi Dodoma ili kuboresha yale mapungufu machache yaliyobainika na kuhakikisha miundombinu inakuwa salama na rafiki kwa kila Mtanzania na kuwarahisishia wananchi kufika kwa wepesi, na niwasihi mtunze miundombinu hii bila kuiharibu,” ameeleza CPA Suluo.

Aidha ameeleza kuwa, LATRA imepanga nauli za SGR kwa watu wazima na watoto kuanzia umri wa miaka minne hadi 12 ambazo ni nafuu kwa kila Mtanzania.

Ni jukumu letu kupanga nauli za usafiri huu na kwa daraja la kawaida tumewazingatia Wananchi wa kawaida kwani watazimudu nauli hizi ambapo kwa treni itakayokuwa inasimama kila kituo ni shilingi 13,000 kuanzia Dar es Salaam hadi Morogoro na shilingi 31,000 kuanzia Dar es Salaam hadi Dodoma ambapo watoto chini ya miaka minne hawatalipia gharama hizo na watoto wenye umri wa miaka minne hadi 12 watalipia nusu gharama ya nauli hizo

>>>Inatoka Uk. 08

na nauli hizi zipo katika tovuti yetu www.latra.go.tz," ameeleza CPA Suluo

Ameongeza kuwa "Treni hii iliyokuja leo ni ya haraka yaani (express), hii nayo ina nauli yake na inasimama vituo viwili tu yanii Morogoro na Dodoma na nauli yake ni Shilingi 22,000 kutoka Dar es Salaam hadi Morogoro, na shilingi 50,000 kutoka Dar es Salaam hadi Dodoma lakini TRC wanatoza 40,000 na hawatakiwi kushusha zaidi ya hapo,' aliongeza.

LATRA inaendelea kushirikiana na wadau wengine wa usafiri ili kuhakikisha huduma bora na salama kwa wananchi wote. Uzinduzi wa safari hii mpya ni sehemu ya juhudi za serikali kuboresha sekta ya usafiri na kuunganisha miji mikubwa nchini.

> **"LATRA inaendelea kushirikiana na wadau wengine wa usafiri ili kuhakikisha huduma bora na salama kwa wananchi wote"**
>
> *CPA HABIBU SULUO*


# LATRA YAKANUSHA TUHUMA ZA RUSHWA MOROGORO

Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) imetolea ufafanuzi tuhuma za rushwa zilizosambaa katika mitandao ya kijamii Julai 17, 2024 zikihusisha utoaji leseni za LATRA kwa pikipiki za magurudumu mawili na matatu (Bodaboda na Bajaji) mkoa wa Morogoro ambapo wamiliki wamelalamika kutishwa na kuombwa rushwa ili kupatiwa leseni za LATRA.

Bw. Salum Pazzy, Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano LATRA amefafanua tuhuma hizo kuwa, "LATRA imeona taarifa hiyo iliyosambaa kupitia mitandao ya kijamii ikimuainisha Afisa anayejulikana kwa jina la Fadhili anawalazimisha Madereva wampe fedha awalipie Faini na Stika za LATRA kwa madai mfumo unasumbua, Mamlaka imechukua hatua stahiki kwa haraka ili kupata ufumbuzi wa taarifa hiyo" amesema Bw. Pazzy

Aidha Bw. Pazzy ameeleza kuwa Mamlaka imewasiliana na Ofisi ya Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro na kupata ufafanuzi zaidi juu ya tuhuma hizo ambapo Ofisi hiyo imeeleza kuwa imepokea tuhuma hizo na kuchukua hatua za uchunguzi juu ya mtuhumiwa.

"Afisa anayetuhumiwa ni Bw. Fadhili Elieza, Mwajiriwa wa muda mfupi (temporary staff) katika Halmashauri yetu idara ya ukusanyaji mapato



# LATRA YAKANUSHA TUHUMA ZA RUSHWA MOROGORO




*Bw. Salum Pazzy, Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) (wa katikati) akitoa ufafanuzi kwa waandishi wa habari juu ya tuhuma za rushwa zilizosambaa katika mitandao ya kijamii Julai 17, 2024 zikihusisha utoaji leseni za LATRA kwa pikipiki za magurudumu mawili na matatu (Bodaboda na Bajaji) mkoa wa Morogoro.*

**>>>Inatoka Uk. 09**

na tumemsimamisha kazi mtuhumiwa huyo kupisha uchunguzi ufanyike hadi pale tutakapo jiridhisha ukweli juu ya tuhuma hizo na hatua stahiki zitachukuliwa endapo ukweli utabainika," imeeleza ofisi ya Mkurugenzi wa Halmashauri ya Morogoro.

Kwa upande wake Bw. Omary Mpulila, Katibu wa Umoja wa Wamiliki wa Bajaji Mkoa wa Morogoro ameieleza LATRA kuwa Umoja huo haujawahi kupokea malalamiko hayo kutoka kwa wanachama wake.

"Umoja wetu haujawahi kupokea malalamiko ya wanachama wake kutishwa au kuombwa rushwa wanapohitaji leseni za LATRA, nashauri taarifa hizo zinapaswa kuchunguzwa kwa umakini zisiichafue LATRA inavyoboresha huduma zake kwa wateja kwa uwazi na bila vishawishi vya rushwa," ameeleza Bw. Mpulila.

LATRA ina Hati ya Maelewano (MoU) inayoiwezesha Halmashauri Kutoa Leseni za LATRA kwa Pikipiki za Magurudumu Mawili na Matatu (Bodaboda na Bajaji), Mamlaka inakemea vikali vitendo vyote vya rushwa katika utoaji wa huduma zake, na inatoa wito kwa wadau wake na wananchi wote kutoa taarifa za vitendo vya rushwa kupitia namba 0800110019/20 bila malipo, zinazofanya kazi siku zote saa 24.

> **"Umoja wetu haujawahi kupokea malalamiko ya wanachama wake kutishwa au kuombwa rushwa wanapohitaji leseni za LATRA"**
>
> ***BW. OMARY MPULILLA***



# LATRA YAWATAKA WADAU KUTEKELEZA KANUNI ZA MFUMO WA VTS

Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) imewataka watoa huduma wa vifaa vya kufuatilia mwenendo wa vyombo vya usafiri (VTD) kutekeleza Kanuni za Mfumo wa Ufuatiliaji Mwenendo wa Vyombo vya Usafiri (VTS) za Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini za Mwaka 2024 ili kuboresha huduma za usafirishaji pamoja na kusambaza vifaa vya VTD vyenye ubora na tija katika sekta ya usafirishaji.

Hayo yamebainishwa na Bi. Halima Lutavi, Meneja Ufuatiliaji Usafiri wa Barabara LATRA alipotoa elimu ya Kanuni za VTS kwa watoa huduma wa VTD katika kikao cha pamoja kati ya LATRA na watoa huduma hao kilichofanyika katika ofisi za LATRA Mkoa wa Dar es Salaam Julai 26, 2024.

Aidha, Bi. Halima amesema watoa huduma hao wa VTD wamepitishwa kwenye maeneo yote ya Kanuni hizo za VTS kwa lengo la kuwaongezea uelewa ili watekeleze majukumu yao kwa uweledi na ufanisi kama inavyoelekezwa kwenye Kanuni hizo.

Vilevile Bi. Lutavi amewaasa watoa huduma hao kuendelea kuzisoma na kuzielewa vizuri Kanuni hizo na amesisitiza kuwa, endapo Mamlaka itabaini kuwa Kanuni hizo hazifuatwi, itachukua hatua stahiki ikiwa ni pamoja na kumsimamishia mtoa huduma.

“Hakikisheni mnakuwa na mafundi wenye uweledi na uzoefu ili waweze kuhudumia kifaa kwa ufanisi wa hali ya juu na pia muhakikishe mafundi wenu wana sare na kitambulisho ili waweze kutambulika pale wanapotakiwa kutoa huduma”, ameeleza Bi. Halima.

Aidha, ameongeza kuwa, “Mamlaka inawakaribisha watoa huduma kutoka kampuni mbalimbali ambazo zina uwezo wa kutoa huduma hiyo kwa ufanisi na wanaweza wakafanya maombi ya cheti cha idhini kutoka LATRA kwa kuzingatia vigezo vilivyowekwa na baada ya Mamlaka kujiridhisha kuwa mtoa huduma anaweza kufanya kazi kwa weledi basi ataidhinishwa na kupatiwa cheti cha idhini ya kutoa huduma hiyo.”

Naye. Bw. Geofrey Silanda, Meneja Uratibu Usalama na Mazingira LATRA amesema kuwa, Mamlaka imejipanga kuwasimamia na kufanya ufuatiliaji wa karibu kwa watoa huduma wa vifaa vya VTD, “Sisi kama Mamlaka tutahakikisha tunakagua vifaa hivi vizuri na tukigundua kuwa vifaa havifanyi kazi baada ya kuvifanyia majaribio Mamlaka itampatia mtoa huduma huyo siku 14 kubadilisha kifaa na kukifanyia marekebisho na akishindwa kufanya hivyo tutampa siku 30 na akishindwa kutekeleza basi Mamlaka haitompatia kibali cha kufunga kifaa hicho.”

Kwa upande wake, Wakili Abasi Msuya kutoka TERA Tecknologies ameishukuru Mamlaka kwa ushirikiano mzuri uliopo na kwa kupatiwa elimu ya Kanuni hizo ambazo zitakuwa ni nyenzo nzuri wanapotekeleza majukumu yao, na amewasihi watoa huduma za VTD kuzingatia Kanuni zilizowekwa.

Naye Bw. Christopher Mbagwa, Kaimu Mkuu wa Chuo cha Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi Dar es Salaam (VETA) amesema kuwa, kupitia Kanuni hizi itasaidia kutatua changamoto zinazojitokeza barabarani kwani itasaidia pia uwepo wa mafundi wenye uweledi.

“Nimepokea elimu hii kwa mtazamo chanya ukizingatia usafiri ni jambo muhimu kwa kila Mtanzania na zipo changamoto nyingi zinajitokeza barabarani hivyo kupitia Kanuni hizi changamoto zitatatuliwa na sisi VETA tutawawezesha mafundi kuwa na ujuzi mzuri wa kutengeneza vifaa hivi, vilevile ninawaasa wasambazaji wa vifaa hivi kutumia vifaa vyenye ubora,” amesema Bw. Mbagwa.

# NAIBU KATIBU MKUU - UCHUKUZI AAGIZA MICHEZO KUIMARISHWA

Dkt. Ally Possi, Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Uchukuzi amewaagiza wakuu wa idara za Raslimali watu na Utawala wa taasisi zote za Wizara hiyo kuhakikisha wanaendeleza michezo sambamba na kuongeza ushiriki wa wafanyakazi katika michezo ili timu ya Uchukuzi iendelee kushinda katika mashindano mbalimbali ya baadae na kunufaika na faida za michezo kwa afya za wafanyakazi kama inavyoelekezwa na Serikali.

Ameyasema hayo jana tarehe 27 Julai, 2024 jijini Dodoma katika ufunguzi wa Bonanza maalum la Wizara ya Uchukuzi lililoandaliwa na Shirika la Reli Tanzania (TRC) ikiwa ni sehemu ya hamasa ya ufunguzi wa huduma za Treni za umeme za Reli ya Kisasa (SGR) Dar es Salaam hadi Dodoma. ambapo Dkt. Possi alikuwa mgeni Rasmi.

"Michezo ni sehemu ya maelekezo ya Serikali, tuendeleze michezo ili tuimarishe afya zetu na kuongeza uwezo wetu wa kuchapa kazi. Bonanza linalofuata la Uchukuzi litafanyika jijini Mwanza na mwenyeji wetu atakuwa ni Kampuni ya Huduma za Meli (MSCL), ni muhimu tujipange mapema na mimi mwenyewe nitashiriki kucheza mchezo wa riadha," alisema

Aidha ametoa pongezi kwa TRC na Uongozi wa Klabu ya Uchukuzi kwa kuwezesha bonanza hilo lililoratibiwa vizuri na kuwezesha wafanyakazi waliojitokeza kwa wingi kushiriki michezo mbalimbali iliyoandaliwa ikiwemo mpira wa miguu, mpira wa pete, kuvuta kamba, michezo ya jadi, riadha na mingineyo.

"Natoa pongezi kwa wenzetu wa TRC na uongozi wa klabu ya uchukuzi na kamati nzima iliyowezesha bonanza hili, kiupekee nampongeza mwenyekiti wa klabu hii Bw. Andrew Magombana, huyu ni mwanamichezo mzoefu

>>>Inaendelea Uk. 13



*Dkt. Ally Possi, Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Uchukuzi, akimkabidhi CPA Habibu Suluo, Mkurugenzi Mkuu Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) kombe maalumu la Mkuu wa Taasisi ambaye amewezesha wafanyakazi wengi zaidi kuhudhuria bonanza la Wizara ya Uchukuzi lililoandaliwa na Shirika la Reli Tanzania (TRC) jijini Dodoma 27 Julai, 2024.*



*CPA Habibu Suluo, Mkurugenzi Mkuu Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) akishiriki bonanza maalum la Wizara ya Uchukuzi lililoandaliwa na Shirika la Reli Tanzania (TRC) jijini Dodoma 27 Julai, 2024.*

>>>**Inatoka Uk. 12**

na anayo historia nzuri ya kusimamia michezo," aliongeza

Katika bonanza hilo, Dkt. Possi alitoa medali na vikombe kwa washindi wa michezo iliyochezwa ambapo kwa mpira wa miguu timu ya TRC imepokea kombe la mshindi wa kwanza, kwa mchezo wa kuvuta Kamba wanaume, timu ya Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) iliyoshirikiana na timu ya Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania (TASAC) wamepokea kombe la mshindi wa kwanza na Kamba wanawake timu ya wizara ya Uchukuzi imepokea kombe la mshindi wa kwanza.

Katika utoaji wa vikombe hivyo, CPA Habibu J. Suluo, Mkurugenzi Mkuu LATRA amekabidhiwa na Mgeni Rasmi kombe maalum kwa kuwa Mkuu wa Taasisi aliyewezesha wafanyakazi wengi zaidi kuhudhuria bonanza hilo na yeye mwenyewe kushiriki kikamilifu katika michezo mara kwa mara.

Wachezaji wengine waliokabidhiwa medali ni pamoja na Stamil Mbilu wa Wizara ya Uchukuzi aliyekuwa mshindi wa kwanza kwa mbio za magunia wanawake, Abdul Ukenge wa TRC aliyeibuka mshindi wa kwanza kwa riadha mita 100, Lugano Mwasomola wa LATRA aliyeibuka mshindi wa pili riadha mita 100. Pia Mwasomola amekabidhiwa medali ya mfungaji bora wa mchezo wa mpira wa miguu.

Kwa upande wake, CPA Habibu J. Suluo, Mkurugenzi Mkuu wa LATRA ametoa pongezi kwa TRC na Klabu ya Wizara ya Uchukuzi kwa kuandaa bonanza hilo kwa ufanisi mkubwa na amewasihi wanamichezo kuendeleza umoja wao hadi katika utendaji wa kazi za ofisini ili kuongeza tija katika utendaji wa taasisi zao.

"Mimi nimekuwa nikishiriki michezo hii mwenyewe bila kutuma muwakilishi, hii ni kwa sababu ninaipa michezo kipaumbele kwa kuwa michezo ni afya, michezo ni umoja na hivyo inaimarisha utendaji wa kazi hadi za ofisini," alisema

Katika hatua nyingine, CPA Suluo ameupongeza

>>>**Inaendelea Uk. 14**

>>>Inatoka Uk. 13

uongozi wa TRC kwa kazi nzuri inayoendelea kufanyika katika kutoa huduma za treni ya SGR na kuongeza kuwa, LATRA imepanga nauli inayowalinda watumia huduma wenye kipato cha chini wanaolazimika kutumia daraja la kawaida wanaposafiri na treni hizo, kwa madaraja ya juu TRC wanaruhusiwa kutoza nauli yoyote watakayoona inafaa.

"Tunapongeza mazuri yanayofanyika, Serikali inaendelea kuzifanyia kazi changamoto chache zilizopo. Pia napenda nitoe zawadi ya LATRA kwa wadau wanaotumia usafiri wa mabasi, tumieni Mfumo wa Taarifa kwa Abiria (PIS) unaopatikana kwa kuingiza anwani pis.latra.go.tz utaweza kuona yalipo mabasi yanayokuja katika kituo ulichopo, muda wa kufika katika kituo husika na utaweza kukagua mwendo wa basi kwa kuingiza namba ya basi hilo katika mfumo," alifafanua

Pia Dkt. Possi ametoa wito kwa watanzania kutumia usafiri wa treni za SGR kwa kuwa ni huduma nzuri na ya gharama nafuu inayowawezesha watu wenye vipato tofauti tofauti kutumia usafiri huo.

"Binafsi nimetumia usafiri wa SGR, ni gharama nafuu na haraka hata ukilinganisha na usafiri wa anga, kuna tofauti kubwa ya gharama. Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, inayoongozwa na Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan inaendelea kuwekeza katika miundombinu tofauti tofauti ya uchukuzi, tunayo haki ya kujipongeza," alisema

> **"Binafsi nimetumia usafiri wa SGR, ni gharama nafuu na haraka hata ukilinganisha na usafiri wa anga, kuna tofauti kubwa ya gharama"**
>
> *DKT. ALLY POSSI*



*Wafanyakazi wa Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) wakishiriki mchezo wa kuvuta kamba katika bonanza maalum la Wizara ya Uchukuzi lililoandaliwa na Shirika la Reli Tanzania (TRC) jijini Dodoma 27 Julai, 2024.*

# WANANCHI WAKOSHWA NA LATRA SABASABA



*Wadau mbalimbali wakipatiwa elimu kuhusu kazi na majukumu yanayotekelezwa na Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) walipotembelea jengo la LATRA kwenye Maonesho ya 48 ya Kimataifa ya Biashara (sabasaba) katika viwanja vya Julius Nyerere Julai 1, 2024 Jijini Dar es Salaam*

Wadau mbalimbali wa usafiri nchini wametembelea jengo la Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) na kujifunza kazi na majukumu mbalimbali yanayotekelezwa na LATRA kwenye Maonesho ya 48 ya Kimataifa ya Biashara Dar es Salaam (sabasaba) katika viwanja vya Julius Nyerere yanayoendelea kuanzia Juni 28 hadi Julai 13, 2024.

Akizungumza baada ya kutembelea Jengo la LATRA na kupatiwa elimu kuhusu Mamlaka inavyotekeleza majukumu yake, Bw. Damian Patrick, Mdau wa Usafiri Ardhini na amesema ameridhishwa na huduma zinazotolewa na LATRA na jinsi huduma hizo zinavyokuwa msaada kwa wananchi,

"Kwa kweli, nimeridhishwa na LATRA kwa huduma nzuri wanayotoa katika maonesho haya kwani nimepokelewa vizuri na kujifunza mengi hususan Mifumo yao ya kidigitali ya kufuatilia mwenendo wa mabasi. Pia, huduma za kutoa leseni za usafirishaji kwani wameturahisishia sisi wadau kupata leseni zetu kwa urahisi kupitia mfumo wa maombi ya leseni na kizuri zaidi kwa sasa tunachapa wenyewe leseni na hatuna haja ya kwenda kwenye ofisi zao kufuata leseni," amesema Bw. Patrick.

Kwa upande wake Bi. Neema Mkwera, mdau wa usafiri ameeleza kuwa, "nimejifunza mengi kutoka LATRA na kufahamu kuwa wapo kwa ajili ya kusimamia usalama barabarani kwani wanaweza kudhibiti mwendo wa mabasi wakati wowote na kuhakikisha usalama wa abiria tunapokuwa safarini pamoja na kututoa wasiwasi tunapokuwa safarini."

Naye Bw. Chilo Raphael, mhudumu wa mabasi ya mijini (Daladala) ameonesha kufurahia huduma za LATRA alizozipata katika Jengo hilo ikiwa ni pamoja na kuwasilisha changamoto za usafiri jijini Dar es Salaam.

"Nafurahishwa na usimamizi mzuri wa LATRA katika sekta ya usafirishaji, naiomba Mamlaka kwa niaba ya makondakta wenzangu kutusaidia kusafirisha abiria kwa urahisi bila changamoto zozote hasa kutuongezea vituo vya kuwashusha abiria kwani hili swala limekuwa kilio chetu kikubwa," ameeleza Bw. Raphael.

Naye Bw. Johansen Kahatano, Mkurugenzi Udhibiti Usafiri wa Barabara LATRA amewashukuru wadau mbalimbali waliotembelea jengo la LATRA kwa kujifunza mengi kuhusu Mamlaka.

"Nawashukuru wadau na viongozi mbalimbali waliotutembelea hapa sabasaba kwa lengo la kufahamu kazi na majukumu tunayoyatekeleza kwani wameshuhudia mengi kuhusu Mamlaka na wametushauri maeneo ya kuboresha ili kwa pamoja tuwe na sekta ya usafiri ardhini yenye tija kwa wananchi, wasafirishaji pamoja na Serikali."

Katika maonesho ya 48 ya Kimataifa ya Biashara (sabasaba), wananchi wanapata fursa ya kujifunza masuala mbalimbali yahusuyo usafiri ardhini ikiwa ni pamoja na matumizi ya Mfumo wa Kufuatilia Mwenendo wa Magari (VTS) na mfumo mpya wa Taarifa kwa Abiria (PIS – Passenger Information System).

# HABARI PICHA




*Bw. Athumani Kwikima, Mkurugenzi wa Huduma za Mamlaka (wapili kushoto) akipokea tuzo ya LATRA ya mshindi wa pili katika kundi la Mamlaka za Udhibiti, zilizotolewa na Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara (TANTRADE) katika viwanja vya Julius Nyerere kwenye hafla ya kufunga maonesho ya 48 ya Kimataifa ya Biashara (sabasaba) jijini Dar es Salaam Julai 13, 2024.*




*CPA, Habibu Suluo, Mkurugenzi Mkuu LATRA, (wa pili kushoto), na Bw. Kiseo Yusuf Nzowa, Katibu Tawala Mkoa wa Kilimanjaro, (wa tatu kushoto) waki kabidhi hundi ya mfano kwa Chama cha Ushirika Mikopo na Akiba cha Bajaji na Bodaboda mkoani Kilimanjaro (KIBABOT SACCOS) ikiwa ni sehemu ya gawio ya 20% ya leseni zilizotolewa na chama hicho kwa niaba ya LATRA Septemba 03, 2024 katika Ukumbi wa Mikutano ofisi ya Mkuu wa Mkoa – Kilimanjaro.*

*Mha. Hanya Mbawala, Mkurugenzi Udhibiti Usafiri wa Reli wa Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) (wa tatu kulia), akiambatana na Bw. Bahati Shagihilu, Afisa Usafirishaji Wizara ya Uchukuzi (wa kwanza kushoto), Mha. David Matiko kutoka Shirika la Reli Tanzania (TRC) (wa pili kulia) pamoja na Maafisa Wakaguzi wa Reli kutoka LATRA wakiwemo Mha. Medani Ndabagoye (wapili kushoto) na Mha. Michael Mwachiko (wa kwanza kulia) wakikagua usalama wa reli ya kati kuanzia Tabora hadi Mpanda Mkoani Katavi Septemba 25, 2024.*



# LATRA YAPONGEZWA UBUNIFU WA MIFUMO YA TEHAMA

Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) imepongezwa kwa kubuni Mifumo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) na kuitumia mifumo hiyo katika utendaji kazi wa kila siku jambo linaloongeza ufanisi wa utoaji huduma kwa wadau wake.

Pongezi hizo zimetolewa na Dkt. Ladislaus Chang'a, Kaimu Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) alipotembelea banda la LATRA, viwanja vya Nzuguni - Dodoma kwenye Maonesho ya Kilimo ya Kimataifa – Nanenane, Agosti 6, 2024.

Dkt. Chang'a amesema, "Nawapongeza kwa kubuni Mfumo wa Kufuatilia Mwenendo wa Magari (VTS) pamoja na Mfumo wa Taarifa kwa Abiria (PIS) uliotengenezwa na wataalam wetu wa ndani na umekuwa na manufaa makubwa kwa Serikali, Wasafirishaji na Wananchi kwa ujumla."

Naye Bw. Hamza Johari, Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania (TCAA), ameipongeza LATRA kwa kazi nzuri ya kiudhibiti inayoifanya kwa kuwa suala zima la usalama wa usafiri ardhini umeongezeka na unaridhisha.

"Tumeshuhudia usalama wa usafiri ardhini kwa maana ya usafiri wa barabara na pia kwa usafiri wa reli ambao kwa sasa tumeona usafiri kwa treni ya kisasa ya SGR umeanza kwa kasi katika Taifa letu na hiki ni kielelezo tosha kwamba LATRA inatekeleza majukumu yake kwa kiwango cha hali ya juu," ameeleza Bw. Johari.

Vilevile Bw. Johari, amesema amefurahishwa na Mfumo wa PIS unaomwezesha mwananchi kuangalia mwendokasi wa basi alilopanda na endapo basi husika lina mwendo hatarishi, anawasiliana na LATRA kwa kuwapigia simu na wao wanashughulikia jambo hilo kwa wakati.

Tumeshudia uboreshaji wa huduma mbalimbali kimtandao kama vile matumizi ya Mfumo wa Tiketi Mtandao ambapo kwa sasa unaweza kununua tiketi kupitia simu yako janja ya mkononi popote ulipo, kwa wakati wowote na kufanya wekesho (booking) bila kulazimika kwenda kituo cha mabasi kufuata huduma hiyo, haya ni maendeleo makubwa sana," amesema Bw. Johari,

Wadau mbalimbali waliotembelea banda la LATRA kwenye Maonesho ya Nanenane - Dodoma wameeleza kuwa kwa sasa huduma

>>>Inaendelea Uk. 18



*Bw. Hamza Johari Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania (TCAA) akipata maelezo ya Mfumo wa Taarifa za Abiria (PIS) unavyofanya kazi alipotembelea banda la LATRA viwanja vya Nzuguni jijini Dodoma kwenye Maonesho ya Kilimo ya Kimataifa - Nanenane Agosti 01, 2024.*



*Mha. Eliud Kataraihya, Mkuu wa idara ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) wa Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) akitoa elimu ya Mifumo ya TEHAMA kwenye Maonesho ya Kilimo ya Kimataifa – Nanenane jijini Dodoma Agosti 02, 2024.*

**>>>Inatoka Uk. 17**

za usafiri ardhini zimerahisishwa kama vile kwa kutumia Mfumo wa PIS, wanafuatilia vituo vya mabasi pamoja na kufahamu muda mwafaka wa kuwasili kule wanakoenda na hata kama wana ndugu anayetoka mkoa mwingine, wanatazama kwenye mfumo na kuona muda atakaofika.

Bi. Alicia Sebastian, ni mmoja wa wadau na anaeleza kuwa, kupitia maonesho hayo amejifunza LATRA inavyodhibiti mabasi na vyombo vya usafiri vinavyofanya biashara ardhini pamoja na mifumo ya TEHAMA na jinsi ilivyorahisisha upatikanaji wa taarifa za LATRA na usafiri kwa ujumla.

Kwa upande wake, CPA Habibu Suluo, Mkurugenzi Mkuu LATRA amesema kuwa, LATRA itaendelea kutekeleza jukumu lake la kiudhibiti kwa mujibu wa Sheria, Kanuni na Taratibu za usafiri ardhini zilizowekwa na wataendelea kushirikiana na wadau katika kila hatua ili kuwa na usafiri wa ardhini ulio salama na wenye tija kwa wote.

Pia, amewasihi madereva wa vyombo vya moto vinavyodhibitiwa ambao bado hawajasajiliwa na kuthibitishwa na LATRA wafanye hivyo na amewataka Madereva wote waliothibitishwa kutumia kitufe cha utambuzi wa dereva (i-Button) wakati wote wa safari na kufanya vinginevyo ni kinyume cha Sheria na Kanuni zilizopo na hivyo watachukuliwa hatua stahiki pindi watakapokutwa bila kitufe hicho.

Mamlaka inashiriki katika Maonesho ya Kilimo ya Kimataifa – Nanenane yanayofanyika viwanja vya Nzuguni - Dodoma kuanzia Agosti 01-08, 2024. LATRA ni mdau mkubwa wa sekta ya Kilimo kwa kuwa ndiyo Taasisi ya Umma inayotoa leseni za usafirishaji inayowezesha usafirishaji wa pembejeo za kilimo na mazao kutoka shambani hadi kwa mlaji.

> **“ LATRA itaendelea kutekeleza jukumu lake la kiudhibiti kwa mujibu wa Sheria, Kanuni na Taratibu za usafiri ardhini ”**
>
> ***CPA HABIBU SULUO***

# MHE. KIHENZILE AIPA TANO LATRA, MFUMO WA PIS

Mhe. David Kihenzile (Mb), Naibu Waziri wa Uchukuzi ameipongeza Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) kwa kubuni Mfumo wa Taarifa kwa Abiria - PIS unaopatokana kwa anwani ya pis.latra.go.tz unaowasaidia abiria na wadau wa usafiri nchini kufahamu taarifa za mabasi yanayoelekea vituo vya mabasi vilivyo karibu yao na kuwawezesha wadau hao kufahamu mwendokasi na mahala lilipo basi husika.

Mhe. Kihenzile ametoa pongezi hizo Agosti 08, 2024, viwanja vya Nzuguni Dodoma alipotembelea banda la LATRA kwenye Maonesho ya Kilimo ya Kimataifa ya Nane Nane na kujionea jinsi Mamlaka hiyo inavyotekeleza majukumu yake ya kiudhibiti kwa mujibu wa Sheria, Taratibu na Kanuni zilizopo.

"Mnastahili pongezi kwa kubuni Mfumo huu ambao unatoa taarifa muhimu kwa abiria ikiwemo kufahamu mwendokasi wa basi husika pamoja na vituo mbalimbali vya mabasi vilivyopo nchini," amesema Mhe. Kihenzile.

Naye Bw. Gerson Msigwa, Katibu Mkuu Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo, alipozulu katika banda la LATRA alifurahishwa na jinsi Mamlaka hiyo inavyotumia fursa za Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) kwa kubuni mifumo madhubuti inayosaidia katika udhibiti wa sekta ya usafiri ardhini pamoja na kurahisisha utoaji wa huduma na taarifa muhimu kwa abiria na wasafirishaji kwa jumla.

Miongoni mwa mifumo aliyoizungumzia ni Mfumo wa PIS ambapo baada ya kupatiwa maelezo ya jinsi mfumo huo unavyofanya kazi, Bw Msigwa alisema kuwa, kutokana na umuhimu wa mfumo huo kwa wananchi, ni vema Mamlaka ikaongeza juhudi za kuutangaza zaidi ili uweze kufahamika kwa wananchi ambao ndio walengwa wakuu wa mfumo ukizingatia kuwa ni mfumo rahisi kuutumia.

Kwa upande wake, Mha. Eliud Kataraihya, Mkuu wa Kitengo cha TEHAMA - LATRA amesema Mamlaka

>>>Inaendelea Uk. 20



*Mhe. David Kihenzile (Mb), Naibu Waziri wa Uchukuzi akipatiwa elimu ya Mfumo wa Tarifa kwa Abiria (PIS) alipotembelea banda la LATRA kwenye Maonesho ya Kilimo ya Kimataifa – Nanenane jijini Dodoma Agosti 02, 2024.*

# MHE. KIHENZILE AIPA TANO LATRA...

>>>Inatoka Uk. 19

itaendelea kubuni na kutumia mifumo ya TEHAMA na kuhakikisha inasomana kama ilivyoelekezwa na Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania.

Mamlaka imeshiriki katika Maonesho ya Nanenane jijini Dodoma kwa kutoa elimu ya kazi na majukumu ya Mamlaka pamoja na kuonesha Mifumo mbalimbali ya TEHAMA inayotumika na Mamlaka hiyo ikiwemo Mfumo wa PIS, Mfumo wa Kufuatilia Mwenendo wa Magari (VTS), Mfumo Tumizi wa LATRA App, Mfumo wa Tiketi Mtandao pamoja na Mfumo wa Utoaji wa Leseni (RRIMS).






*Bw. Gerson Msigwa, Katibu Mkuu Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo, akipatiwa elimu ya Mfumo wa PIS na Bw. Ezekiel Emmanuely, Afisa Mfawidhi Mkoa wa Dodoma katika banda la LATRA kwenye Maonesho ya Kilimo ya Kimataifa – Nanenane jijini Dodoma Agosti 02, 2024.*

# DISEMBA 31, 2024 MWISHO WA KUTUMIA WAHUDUMU WA MABASI WASIOSAJILIWA

Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) imewasihi watoa huduma za usafiri wa magari ya abiria ya masafa marefu kuwahimiza wahudumu waliowaajiri kupata mafunzo kutoka Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT) au Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE), na tarehe 31 Disemba, 2024 ndio mwisho kwa wasafirishaji kutumia wahudumu ambao hawajasajiliwa na LATRA.




Hayo yamebainishwa na Bw. Salum Pazzy, Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano - LATRA alipozungumza na vyombo vya habari katika ukumbi wa mikutano ofisi za LATRA Dar es Salaam Agosti 14, 2024.

Aidha, Bw. Pazzy ameongeza kuwa, baada ya mafunzo, wahudumu hao watatakiwa kuwasilisha maombi ya kusajiliwa LATRA kwa mujibu wa taratibu zilizopo kupitia Mfumo wa Maombi ya Leseni za Usafirishaji (RRIMS) unaopatikana kwa anwani ya https://rrims.latra.go.tz/login ili kupatiwa kadi ya usajili ya mhudumu kwa mabasi ya abiria,

"Mamlaka inawakumbusha wahudumu wote ambao wamepata mafunzo, kutuma maombi ya kusajiliwa kupitia https://rrims.latra.go.tz/login kwa kutumia Namba ya Kitambulisho cha Taifa (NIDA) au kufika ofisi yoyote ya LATRA. Maombi yaambatishwe na Cheti cha mafunzo na picha mbili za pasipoti zenye kivuli cheupe," amesisitiza Bw. Pazzy.

Vilevile, Bw. Pazzy amezitaja faida za wahudumu kusajiliwa na LATRA kuwa itasaidia kurasimisha fani na ajira zao, kuongeza uwajibikaji katika kutoa huduma kwa mujibu wa Sheria pamoja na kujenga ari ya umoja na mshkamano wa wahudumu hao katika masuala ya haki na wajibu wao .

Kwa upande wake Dkt. Nasibu Mramba, Kaimu Naibu Mkuu wa Chuo - CBE ameeleza kuwa, uongozi wa CBE unashirikiana na LATRA na wadau wengine kuwapatia mafunzo wahudumu wa mabasi ya masafa marefu kwenye maeneo ya Kanuni, Sheria na maadili ya usafirishaji wa abiria pamoja na usalama ili kuhakikisha abiria wanapatiwa huduma bora.

Naye Bi. Honesta Mjaki, Mratibu wa Mafunzo ya Watoa Huduma - NIT, ameeleza kuwa, Chuo cha NIT kimetoa mafunzo kwa wahudumu 503 na kimewafikia wahudumu wa kampuni mbalimbali Tanzania Bara na amewasihi wahudumu kujitokeza kwa wingi kupatiwa mafunzo.

Kwa mujibu wa Kifungu cha 5(1)(e) cha Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini Sura ya 413, Mamlaka ina jukumu la kusajili wahudumu

>>>Inaendelea Uk. 22

>>>Inatoka Uk. 21

## DISEMBA 31, 2024 MWISHO WA KUTUMIA WAHUDUMU....

na kuthibitisha madereva wa vyombo vya moto vinavyotoa huduma za usafiri kibiashara. Pia, Kanuni ya 17 ya Kanuni za Uthibitishaji Madereva na Usajili Wahudumu wa Magari ya Biashara za Mamlaka ya Udhibiti usafiri Ardhini (LATRA) za mwaka 2020, zinamtaka mtu yeyote anayekusudia kufanya kazi ya uhudumu katika gari linalotoa huduma za usafiri kibiashara kusajiliwa na LATRA.

> "Mamlaka inawakumbusha wahudumu wote ambao wamepata mafunzo, kutuma maombi ya kusajiliwa kupitia https://rrims.latra.go.tz/login
>
> *BW. SALUM PAZZY*

# BW. PAZZY: WAPIGIENI KURA WASAFIRISHAJI BORA WA MABASI

Bw. Salum Pazzy, Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano, Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) amewasihi wadau wa usafiri ardhini kupiga kura kwa kujaza dodoso kupitia kiunganishi https://forms.edodoso.gov.go.tz/x/Othf4u0Q ili kuchagua wasafirishaji bora na salama wa mabasi ya masafa marefu nchini na yanayoenda nchi jirani, na mwisho wa kupiga kura ni tarehe 19 Agosti, 2024.

Akizungumza na wanahabari Agosti 14, 2024 katika ofisi za LATRA Mkoa wa Dar es Salaam, Bw. Pazzy amesema kuwa, Mamlaka imeandaa tuzo za LATRA kwa Wasafirishaji Bora na Salama kwa Mabasi ya Mikoani na Nchi Jirani ili kuhamasisha na kuchochea matumizi ya mifumo ya utoaji wa huduma bora na salama ya usafirishaji wa abiria kwa ufanisi na ubunifu hususan katika matumizi ya teknolojia.

Vilevile amesema, Mamlaka imeandaa tuzo za Wasafirishaji Bora na Salama kwa huduma za mabasi zilizotolewa kuanzia tarehe 01 Julai 2023 hadi 30 Juni 2024 na Washindi watakabidhiwa tuzo katika Maadhimisho ya Wiki ya Nenda kwa Usalama Barabarani yatakayofanyika tarehe 26 hadi 30 Agosti 2024 Mkoani Dodoma.

>>>Inaendelea Uk. 23



>>>Inatoka Uk. 22

## BW. PAZZY: WAPIGIENI KURA...

Aidha, Bw. Pazzy ameeleza kuwa Mamlaka itazingatia vigezo mbalimbali vitakavyotumika kupata washindi ikiwemo usalama wa huduma inayotolewa, uhakika wa huduma inayotolewa, ubunifu na matumizi ya teknolojia katika utoaji huduma ambayo itawafurahisha abiria na msafirishaji anayetoa huduma iliyokuwa endelevu na uhakika kwa abiria.

"Watumia huduma na wadau wote mnaombwa kushiriki kwa kuwapigia kura wasafirishaji kwa kuzingatia huduma zilizotolewa kwa kipindi husika. Vigezo na jinsi ya kupiga kura vinapatikana kupitia tovuti ya Mamlaka www.latra.go.tz kurasa za mitandao ya kijamii za LATRA au kiunganishi https://forms.edodoso.gov.go.tz/x/Othf4u0Q," amesisitiza Bw. Pazzy.

Vilevile amefafanua kuwa, washindani wamegawanywa katika makundi matatu ambayo ni Wasafirishaji Wakubwa (wenye mabasi zaidi ya 30), Wasafirishaji wa Kati (wenye mabasi 11 hadi 30) na Wasafirishaji Wadogo (wenye mabasi matatu hadi 10).

Kifungu cha 6(a) cha Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini Sura ya 413, pamoja na mambo mengine, kinaeleza kuwa Mamlaka ina wajibu wa kuhamasisha ushindani wenye ufanisi miongoni mwa watoa huduma zinazodhibitiwa, na uandaaji wa tuzo hizo ni sehemu ya utekelezaji wa jukumu hilo.

## MHE. PROF. MBARAWA: SERIKALI KUFUNGUA NCHI NA KUBORESHA MIUNDOMBINU KATIKA SEKTA YA UCHUKUZI

Mhe. Prof. Makame M. Mbarawa (Mb) Waziri wa Uchukuzi, amesema Serikali inaendelea kujenga, kuboresha miundombinu ya uchukuzi na kufanya mabadiliko ya kimkakati katika sekta ya uchukuzi ili kufungua nchi na Mataifa mengine.

Mhe. Prof. Mbarawa ameyasema hayo, tarehe 14 Agosti, 2024 katika Ukumbi wa Mikutano wa Johari Rotana, jijini Dar es Salaam wakati akifungua Mkutano wa Tano wa Kimataifa wa Uchukuzi ulioandaliwa na Chama cha Wasafirishaji Mizigo cha Jumuiya ya Afrika Mashariki (FEAFFA).

Mhe. Prof. Mbarawa ametumia fursa hiyo kuwaomba wadau wa sekta binafsi kuungana ili kuchangamkia fursa lukuki katika sekta ya Uchukuzi.

> **"Serikali imefanya marekebisho ya sheria namba 10 ya mwaka 2017 ili kuruhusu ushiriki wa sekta binafsi katika kutoa huduma kwa njia ya reli"**
>
> *Prof. Makame Mbarawa (Mb)*

"Serikali imefanya marekebisho ya sheria namba 10 ya mwaka 2017 ili kuruhusu ushiriki wa sekta binafsi katika kutoa huduma kwa njia ya reli, hivyo pamoja na Shirika la Reli Tanzania (TRC) kutoa huduma za reli, sekta binafsi inakaribishwa kutoa huduma hiyo ili kuhakikisha wateja wananufaika na miundombinu hiyo, mwekezaji tunamkaribisha aje na vichwa vyake pamoja na mabehewa yake kutumia reli ya kisasa (SGR) na tunaamini TRC pekee hatoweza kutoa huduma peke yake, hivyo tunaamini kwa kushirkiana na mashirika binafsi tunaweza tukaona mabadiliko makubwa katika sekta ya usafiri na usafirishaji" ameeleza Mhe. Prof. Mbarawa.

Aidha amesema mkutano huo umekusudia kujenga ushirikiano wa pamoja katika sekta ya uchukuzi, kuweka

>>>Inaendelea Uk. 24




*Prof. Makame M. Mbarawa (Mb), Waziri wa Uchukuzi akisoma hotuba wakati wa ufunguzi wa Mkutano wa Tano wa Kimataifa wa Uchukuzi ulioandaliwa na Chama cha Wasafirishaji Mizigo cha Jumuiya ya Afrika Mashariki (FEAFFA) Agosti 4, 2024 katika Ukumbi wa Mikutano wa Johari Rotana Jijii Dar es Salaam.*

>>>Inatoka Uk. 23

# SERIKALI KUFUNGUA NCHI NA KUBORESHA MIUNDOMBINU

fursa ya kuongeza ufahamu, kutathmini maendeleo ya kimataifa na maendeleo ambayo Afrika na hasa kanda ya Afrika Mashariki imefanya, kuangazia vikwazo na kupendekeza namna ya kusonga mbele kwenye sekta ambayo ni kitovu cha Uchumi.

"Tanzania kuwa mwenyeji wa mkutano huu ni fursa kubwa kwa uchumi wa nchi kwani Tanzania ni lango kuu kwa kuhudumia mizigo ya nchi saba za wanachama za Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika na hii inatokana na Tanzania kuwa na njia kuu tisa za usafiri wa barabarani kwenye shoroba za ukanda wa TANZAM, wa kaskazini mashariki, kusini pwani kati maziwa makuu, wa kusini, wa magharibi, wa Kati na Ukanda mkuu wa Kaskazini" ameeleza Mhe. Prof. Mbarawa

Vilevile kwa upande wake Rais wa Chama cha Wakala wa Forodha (TAFFA), Bw. Edward Urio amesema kuwa mikutano kama hii ni fursa kwa serikali kuweza kuelezea mipango yake, mikakati yake na pia kupitia wizara ya uchukuzi imewahakikishia wadau wa sekta binafsi kuwa kuna baadhi ya sera zitafanyiwa kazi na zitaleta manufaa kwa nchi.

Aidha Mhe. Prof. Mbarawa ameeleza kuwa kwa upande wa reli ya Shirika la Reli Tanzania (TRC) serikali imeanza kufanya ukarabati wa njia ya reli ya zamani ya (Meter Gauge) kwa kuboresha njia mpya kwa kubadilisha reli nzito na kuimarisha madaraja kati.

"Lengo kuu la serikali ni kuhakikisha reli hiyo ya zamani (meter gauge) inafanya kazi ipasavyo na inachangia kwa kiasi kikubwa sekta ya usafirishaji na logistiki, serikali ya awamu ya sita pia imefanya ujenzi wa reli mpya ya kisasa (SGR) yenye urefu wa kilometer 1219 kwa awamu ya kwanza na awamu ya pili yaani kutoka Dar es salaam mpaka Dodoma nayo imekamilika na nyote ni mashahidi"amefafanua Mhe. Prof. Mbarawa

Mhe. Prof. Mbarawa amefafanua kuwa hadi sasa serikali imeendelea kununua vichwa 19 vya umeme na mabehewa 89 ya abiria na vichwa vya mchongoko 10 na hadi sasa serikali imeshapokea vichwa 17 vya umeme mabehewa 65 ya abiria na seti ya treni ya mchongoko 3.

>>>Inaendelea Uk. 25




>>>Inatoka Uk. 24

"Miradi mingine mitatu ya ujenzi wa reli mpya, zenye reli za kisasa yenye uwezo wa kubeba tani 3,500 kwenye ziwa Tanganyika na nyingine ya kubeba tani 3,000 kwenye ziwa Victoria hivi karibuni zitaanza kujengwa, pia kwa mara ya kwanza kwenye historia ya nchi yetu tunajenga kiwanda kikubwa cha kutengenezea Ndege huko Kigoma, chenye uwezo wa kutengeneza Ndege kubwa yenye uwezo wa kubeba tani 5,000 ambayo naamini ujenzi utaanza hivi karibuni" ameeleza Mhe. Prof. Mbarawa.

Mkutano huo unaofanyika kila mwaka tangu kuanzishwa mwaka 2017, umehudhuriwa na wataalamu wa sekta ya uchukuzi na unajumuisha wanachama wa FEAFFA kutoka nchi za Tanzania, Burundi, Rwanda, Uganda, Kenya na Sudan Kusini, pia nchi ya Afrika kusini na maeneo mbalimbali Duniani.



# MHE. ABDALLAH: AIPONGEZA LATRA KWA UBORA NA UFANISI WA HUDUMA

Kamati ya Mawasiliano Ardhi na Nishati ya Baraza la Wawakilishi Zanzibar imeipongeza Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) kwa ubora na ufanisi wa kutoa huduma kwa wananchi na kwa kushirikiana na Mamlaka ya Usafiri na Usalama Barabarani Zanzibar (ZARTSA), katika utendaji kazi za Usafiri Ardhini.

Mhe. Yahya Abdallah Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano Ardhi na Nishati ya Baraza la Wawakilishi Zanzibar, ameyasema hayo kwenye ziara ya siku moja ya Kamati hiyo ilioambatana na viongozi kutoka Wizara ya Uchukuzi, Wizara ya Ujenzi na Mawasiliano Zanzibar pamoja na Mamlaka ya Usafiri na Usalama Barabarani Zanzibar (ZARTSA), walipoitembelea Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) jijini Dodoma Agosti 29, 2024.

“Kikubwa ambacho tumeweza kukishuhudia sisi ni kuwaona wenzetu walivyopiga hatua kubwa ya ubora na ufanisi wa kutoa huduma zao kwa wananchi lakini kubwa zaidi na la kupendeza ambalo tumeweza kulishuhudia ni kuona jinsi taasisi ya LATRA na ZARTSA kwa upande wa Zanzibar na Serikali ya muungano wanavyoshirikiana katika utendaji wao wa kazi” amesema Mhe. Abdallah.



Aidha Mhe. Abdallah amebainisha kuwa na utofauti wa kisheria baina ya taasisi hizi mbili na kuongeza kuwa LATRA haina Mamlaka kisheria ya kuweza kutoa leseni za udereva kama ilivyo kwa upande wa ZARTSA.

“Ipo haja ya kuangalia hizi sheria na jinsi gani LATRA itaweza kupewa umiliki wa jukumu la kutoa leseni za udereva kisheria moja kwa moja, taasisi zetu zikae ziangalie njia bora ili kuhakikisha changamoto hii inatatuliwa na kuondosha usumbufu kwa wananchi wetu hilo ndo lengo la uwepo wa taasisi hizi” amesisitiza Mhe. Abdallah.

Kwa upande wake, Bw. Abdallah Mhagama, Kaimu Mkurugenzi Mkuu LATRA ameeleza lengo la ziara hiyo ni kujifunza na kubadilishana uzoefu kuhusu udhibiti usafiri ardhini.

“Tuna fursa za kujifunza kutoka bara pamoja na visiwani, kuangalia mbinu tunazotumia huku na mbinu tunazotumia kule, mafanikio pamoja na changamoto

>>>Inaendelea Uk. 27

## MHE. ABDALLAH: AIPONGEZA LATRA KWA UBORA NA UFANISI WA HUDUMA

>>>Inatoka Uk. 26

lakini kikubwa ambacho tumefarijika zaidi ni kwamba waheshimiwa hao wametumia usafiri wa reli ya kisasa (SGR) kutoka Dar es salaam mpaka Dodoma, na wamesifia sana huduma ile na kutupongeza kwa ubunifu tulioufanya kwenye maeneo mbalimbali ya kiudhibiti nchini" ameeleza Bw. Mhagama.

Aidha, Bw. Mhagama, ameihakikishia Kamati hiyo kuwa LATRA itaendelea kutekeleza majukumu yake kwa ukamilifu, na kufanyia kazi ushauri uliotolewa kwa lengo la kuboresha huduma na shughuli zinazofanywa na Mamlaka na kuongeza kuwa ipo haja ya kutengeneza utaratibu ambao msafiri kutoka Zanzibar anaweza akasafiri siku hiyo hiyo na kufika Dodoma.

Vilevile, Mhe. Fatma Ramadhani, Mjumbe wa kamati ya Mawasiliano Ardhi na Nishati ya Baraza la Wawakilishi Zanzibar, ameipongeza LATRA kwa kupiga hatua kwenye upande wa mifumo na kuipongeza serikali ya awamu ya sita inayoongozwa na Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kukamilisha mradi wa reli ya kisasa (SGR).

"Kwanza niwapongeze LATRA kwa upande wa mifumo ya TEHAMA na pia nimpongeze kwa dhati Mama Samia kwa kukamilisha mradi mkubwa wa Reli ya Kisasa (SGR) na mpaka leo tumesafiri kutoka Dar es Salaam kuja Dodoma hatuamini, kwakweli nawapongeza sana ni hatua kubwa imefikiwa na LATRA kiukweli mtu aliyekuwepo nje ya nchi miaka sita akija Tanzania ya leo hawezi kuamini" ameeleza Mhe. Fatma

> **"Nawapongeza sana ni hatua kubwa imefikiwa na LATRA kiukweli mtu aliyekuwepo nje ya nchi miaka sita akija Tanzania ya leo hawezi kuamini**
>
> *MHE. FATMA RAMADHANI*



*Kamati ya Mawasiliano Ardhi na Nishati ya Baraza la Wawakilishi Zanzibar kwenye picha ya pamoja na Menejimenti ya Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA), walipo tembelea ofisi za LATRA Jijini Dododma kwa lengo la kubadilishana uzoefu na kujifunza namna LATRA inavyodhibiti usafiri ardhini nchini, Agosti 29, 2024.*

# BW. NDUHIYE: AITAKA LATRA KUSHIRIKI KIKAMILIFU MABORESHO YA SERA YA TAIFA YA USAFIRISHAJI

Bw. Ludovick Nduhiye, Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Uchukuzi ametembelea Ofisi za Makao Makuu ya Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) jijini Dodoma Septemba 9, 2024, kwa lengo la kujifunza namna LATRA inavyotekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria, Taratibu na Kanuni.

Katika ziara hiyo Bw. Nduhiye ameongoza kikao kilichohudhuriwa na Menejimenti ya LATRA ambapo, CPA Habibu Suluo, Mkurugenzi Mkuu LATRA na wajumbe wa Menejimenti waliwasilisha mada kuhusu utekelezaji wa majukumu ya LATRA na kufafanua mikakati inayotekelezwa na Mamlaka hiyo katika kuboresha huduma za usafiri ardhini nchini.

Akizungumza katika ziara hiyo, Bw. Nduhiye amesema kuwa, amefurahishwa na jinsi LATRA inavyotekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria, Sera na Mipango ya Serikali na kuwa Sekta ya usafiri inapaswa kusimamiwa kwa ufanisi kwa kuwa ni sekta inayoshika uchumi wa nchi.

"Ziara yangu ni ya kujifunza na nitaendelea kujifunza, nimefurahishwa na jinsi LATRA inavyotumia mifumo ya kisasa kuboresha huduma za usafiri ardhini na inavyowafikia wadau kote nchini kwa kuendelea kufungua ofisi mpya kwa baadhi ya Wilaya na maeneo ya kimkakati nchini," alisema Bw. Nduhiye.

Aidha ameitaka LATRA kushiriki kikamilifu katika maboresho ya Sera ya Taifa ya Usafirishaji yanayoendelea kipindi hiki ili sera mpya ihusishe masuala yanayohitajika katika kuboresha utendaji wa Mamlaka hiyo.

Mwishoni mwa ziara hiyo, CPA Suluo alimshukuru Naibu Katibu Mkuu huyo kwa kuitembelea LATRA na alimkabidhi kitabu cha Sheria na Kanuni zinazotumiwa na Mamlaka hiyo kutekeleza majukumu yake ili kumuwezesha kufuatilia zaidi kuhusu kazi zinazotekelezwa na LATRA.




*Bw. Ludovick Nduhiye, Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Uchukuzi akipokea zawadi kutoka kwa CPA Habibu Suluo, Mkurugenzi Mkuu LATRA wakati alipotembelea ofisi za LATRA Jijini Dodoma Septemba 9, 2024.*

# ABOOD, SUPER FEO NA BM WAPEWA SIKU SABA KUJIREKEBISHA



Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) imetoa siku saba kwa mabasi ya Super Feo, Abood Service na BM Coach kujirekibisha haraka kabla hawajasitishiwa leseni zao za kutoa huduma baada ya kubainika kukiuka masharti ya usafirishaji na kusababisha ajali mfululilizo.

Hayo yamebainishwa na CPA Habibu Suluo, Mkurugenzi Mkuu LATRA alipozungumza na waandishi wa habari Septemba 12, 2024 katika ofisi za LATRA Mkoa wa Dar es Salaam.

CPA Suluo amezitaka kampuni hizo kutii Sheria zilizopo ili kuendelea kuboresha utoaji huduma katika sekta ya usafiri ardhini nchini kwani kufanya hivyo kutachochea kupunguza ajali na kuharibika kwa mali.

CPA Suluo ameeleza kuwa, Mamlaka imelazimika kuwaita wamiliki na wasimamizi wa kampuni hizo ili kuwapa nafasi ya kuwasikiliza kabla ya kuchukua hatua za kisheria na kampuni hizo zimeahidi kutii maelekezo waliyopewa.

"Kwa kuwa LATRA imepewa jukumu la kusimamia Sheria na Kanuni zilizopo tumewaita wamiliki wa kampuni hizo kwa ajili ya kuwasilikiliza juu ya hatua tuliyotaka kuichukuwa na wameahidi kuwa watabadilika na kutii Sheria ikiwemo hatua ya kuweka utaratibu wa madereva kuwa wawili katika kila basi ikiwa ni pamoja na kutumia kifaa cha utambuzi (i- Button)" ameeleza CPA Suluo.

Ameongeza kuwa, endapo tabia ya ukiukaji Sheria itakithiri kwa kampuni hizo Mamlaka haitosita kuchukuwa hatua ya kuwatoa katika ratiba za usiku na kuwarudisha katika ratiba za kuanzia saa 11 alfajiri na kuishia saa 6 usiku.

Aidha, CPA Suluo ameeleza kuwa, yapo masharti saba ambayo wasafirishaji hao waliyakubali na kuyasaini kabla ya kupewa kibali cha kutoa huduma ya usafirishaji usiku na kwamba, licha ya makubaliano hayo tayari baadhi yao wameanza kuyakiuka.

Ametaja masharti hayo kuwa ni pamoja na kusaini tamko hilo la LATRA na kulikubali, kuunganisha mabasi kwenye Mfumo wa Kufuatilia Mwenendo wa Magari (VTS), Madereva kupokezana kwenye safari za

>>>Inaendelea Uk. 30

>>>Inatoka Uk. 29

## ABOOD, SUPER FEO, NA BM WAPEWA SIKU SABA KUJIREKEBISHA

zaidi ya saa nane, madereva kusajiliwa na kuthibitishwa na kupewa Kifaa cha Utambuzi (i-botton), kuwa na Ofisa mahsusi ambaye jukumu lake ni kufuatilia mabasi ya kampuni yake, kutoa taarifa sahihi za abiria wanaosafiri, mizigo kuwekwa alama ya utambulisho ya mhusika na kutoruhusu asiye abiria kupanda kwenye gari kabla na wakati wa safari.

"Baadhi ya wasafirishaji wameanza kukiuka masharti hayo na sisi kama LATRA kwa mamlaka tuliyopewa na Sheria, tunatakiwa kuwalinda Watanzania, hatuwezi kuvumilia kuona masharti haya yanakiukwa" amesema CPA Suluo.

Naye Abdallah Kiongozi, Mwenyekiti wa Chama cha Wamiliki wa Mabasi Tanzania (TABOA), ameishukuru LATRA kwa kuzipa kampuni hizo nafasi ya kujirekebisha kutokana na makosa yao.

"Chama chetu hakiko tayari kumtetea msafirishaji anayekwenda kinyume na taratibu za LATRA, na niwasihi wasafirishaji kujirekebisha na kuzingatia Kanuni na Taratibu zilizowekwa" amesema Bw. Kiongozi.

Kwa upande wao wamiliki wa kampuni hizo wameishukuru LATRA na wamekiri makosa yaliyojitokeza na kuahidi kujirekebisha na kutekeleza waliyoagizwa na LATRA. Na wametoa wito kwa wasafirishaji wengine kutii Sheria zilizowekwa na kuomba wananchi kuchagua muda sahihi wa kusafiri wakati wanakata tiketi ili wajue muda wa safari kuanza na wa kufika na kuepusha changamoto zozote ikiwemo kuchelewa kufika kituoni.

> **"Chama chetu hakiko tayari kumtetea msafirishaji anayekwenda kinyume na taratibu za LATRA, na niwasihi wasafirishaji kujirekebisha na kuzingatia Kanuni na Taratibu zilizowekwa"**
>
> *Bw. Abdallah Kiongozi*



# LATRA YASITISHA LESENI YA USAFIRISHAJI KWA KATARAMA LUXURY




*CPA Habibu Suluo, Mkurugenzi Mkuu Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA), akionesha kifaa kilichoharibiwa na Kampuni ya Katarama Luxury wakati wa mkutano na waandishi wa habari kuhusu kusitishwa kwa huduma ya leseni kwa Kampuni ya Katarama Luxury Septemba 12, 2024.*

Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) imesitisha leseni ya usafirishaji kwa mabasi ya kampuni ya Katarama Luxury yanayotoa huduma ya usafiri kwa umma katika mikoa mbalimbali nchini kutokana na kukiuka Kanuni, Sheria na Taratibu za usafirishaji licha ya kuonywa mara nyingi.

Makosa ambayo yamebainika kufanywa ni pamoja na kuondoa kifaa kilichofungwa kwenye mabasi hayo na kufanya ujanja wa kufunga kifaa chao kingine cha kutuma taarifa zisizo sahihi kwenye mfumo wa Kufuatilia Mwenendo wa Magari (VTS).

Hayo yamebainishwa na CPA Habibu Suluo, Mkurugenzi Mkuu LATRA alipozungumza na waandishi wa habari Septemba 12, 2024 katika ofisi za LATRA Mkoa wa Dar es Salaam.

CPA Suluo amesema uamuzi wa kusitisha leseni ya usafirishaji kwa mabasi hayo, umefanyika kwa mujibu wa Kifungu cha 5(1)(b) ya Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini, Sura ya 413 na Kanuni ya 27(1)(c) na (d) ya Kanuni za Leseni za Usafirishaji (Magari ya Abiria) za Mwaka 2020.

"Mtakumbuka kwamba mwaka jana tulimsimamisha kwa kosa la kufanya ushindani usio na tija na kampuni ya Ally's Star, na mwaka huu tulimsimamisha tena kwa kufanya vurugu barabarani na kwa sasa amepiga hatua zaidi kwa kung'oa sehemu ya kifaa kilichothibitishwa na Mamlaka ya Viwango Tanzania (TBS) na kubandika kifaa ambacho kinabadilisha taarifa ya mwendo wa mabasi na amebadilisha kifaa cha antena, kwa hiyo inakuwa haitupi ile taarifa tunayoitegemea, huyu mtu hatuwezi kumvumilia, tumeamua kusitisha leseni ya usafirishaji kwenye mabasi yake yote kuanzia sasa mpaka tumfanyie uchunguzi, na kazi hii itafanywa kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi" amesema CPA Suluo.

Pia, CPA Suluo ameeleza kuwa, Mamlaka kwa kushirikiana na Jeshi la polisi Kikosi cha Usalama Barabarani wanaendelea kufanya uchunguzi na kuanzia Ijumaa Septemba 13, 2024 mabasi ya kampuni hiyo hayatoruhusiwa kutoa huduma yoyote hadi pale uchunguzi utakapokamilika.

CPA Suluo amewasihi na kuwakumbusha watoa huduma za usafiri kuzingatia Sheria na Kanuni katika utoaji wa huduma kwa umma akiwataka kuajiri wahudumu wenye weledi na umahiri na wawapeleke katika mafunzo yanayoendelea kutolewa mikoa mbalimbali kupitia Chuo cha Elimu ya Biashara

>>>Inaendelea Uk. 32

>>>Inatoka Uk. 31

# LATRA YASITISHA LESENI........

(CBE) na Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT).

Naye ACP Nassoro Sisiwayah, Mkuu wa Oparesheni wa Kikosi cha Usalama Barabarani Tanzania, amesema Jeshi la Polisi litahakikisha linafanya uchunguzi wa kina juu ya sababu za mabasi ya Katarama kuendelea kufanya makosa licha ya kuonywa mara kwa mara na LATRA na kuahidi kuchukua hatua baada ya kukamilisha uchunguzi huo.

“Sisi Jeshi la Polisi tutafungua jalada la uchunguzi na uchunguzi utafanyika na kuhoji kupata majibu kamili na endapo tutabaini ni jinai basi tutafungua kesi na aliyefanya kosa hili na wahusika wote watafikishwa mahakamani” amesema ACP Sisiwayah.

Katika hatua nyingine CPA Suluo amesema kuwa, Mamlaka inaendelea kuwasihi wananchi kufuatilia mwenendo wa magari kupitia mfumo wa Taarifa kwa Abiria (PIS) unaopatikana kwa anwani ya https://pis.latra.go.tz kwa kutumia simu janja au kompyuta ili kujua mwendo kasi wa mabasi na kuisaidia Mamlaka kwa kutoa taarifa za mabasi ambayo yatakuwa yanaendesha mwendo hatarishi kupitia namba zinazopatika wakati wote saa 24 ambazo ni 0800110019 au 0800110020.

**“Mamlaka inaendelea kuwasihi wananchi kufuatilia mwenendo wa magari kupitia mfumo wa Taarifa kwa Abiria (PIS)”**

*CPA HABIBU SULUO*



# MABASI SITA YA KATARAMA YAREJESHEWA HUDUMA

Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) imerejesha leseni ya utoaji huduma kwa mabasi sita ya Katarama Luxury kati ya mabasi 10 yaliyositishiwa leseni ya kutoa huduma ya usafirishaji abiria kwa kosa la kubadili sehemu ya Kifaa cha Kufuatilia Mwenendo wa Magari (VTD) na kuweka kifaa kingine kilichosababisha utumaji wa taarifa potofu kwenye Mfumo wa Kufuatilia Mwenendo wa Magari (VTS) mnamo Septemba 13, 2024.

Hayo yamebainishwa na Bw. Salum Pazzy, Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano LATRA kwenye mkutano na waandishi wa habari uliofanyika Septemba 20, 2024 ofisi za LATRA Mkoa wa Dar es Salaam.

Bw. Pazzy amesema kuwa, Mamlaka imefikia uamuzi huo baada ya kufanya uchunguzi wa awali na kubaini kuwa kati ya mabasi 10 mabasi manne ndio yaliyoharibu mfumo huo.

“Katika uchunguzi wa awali kosa lilibainika kwenye mbasi mawili namba T420EDR na T836EDR mara baada ya kusitisha huduma Mamlaka ilifanya uchunguzi kwenye mabasi yote 10 na kubaini mabasi mengine mawili namba T835EDR na T435DXE kuwa yamefanya aina hiyohiyo ya kuingilia mfumo wa VTS, na mabasi hayo yanaendelea kufanyiwa uchunguzi na Jeshi la Polisi” amesema Bw. Pazzy.

Vilevile Bw. Pazzy amebainisha mabasi sita yaliyorejeshewa leseni ya utoaji huduma ambayo yanafanya safari kutoka Dar es Salaam kuelekea Mikoa ya Bukoba na Mwanza kuwa ni, T212ECR, T587EHC, T314 EHW, na T315EHW yanayofanya safari za Mwanza T446EH na T431EHW yanayofanya safari za Bukoba.

Aidha Mamlaka inawakumbusha wasafirishaji wote kuendelea kutii Sheria kanuni na Taratibu zilizopo na Mamlaka inaendelea kufuatilia kwa ukaribu magari yote yaliyopatiwa leseni ya utoaji huduma ya usafirishaji.

“Tunawakumbusha wasafirishaji wote kuwa Mamlaka inaendelea kufuatilia kwa ukaribu magari yote yaliyopewa leseni kwa mujibu wa Sheria na endapo tukabaini uvunjifu wowote wa Sheria, Taratibu na Kanuni au hila zozote ambazo zina haribu utaratibu wowote uliowekwa na kusababisha hasara ambazo hazikuhitajika, Mamlaka haitosita kuchukua hatua kwa msafirishaji yeyote anaevunja taratibu hizo” amesema Bw. Pazzy.

Kwa upande wake Bw. Laurian Katarama, Mmiliki wa Kampuni ya Katarama Luxury, amesema kuwa, watafuata Taratibu na Sheria za Barabarani na kuwaomba radhi abiria kwa usumbufu uliojitokeza baada ya kusitishiwa huduma.

Naye Bw. Elimboto Njoka, Meneja Oparesheni wa kampuni ya Katarama, amesema, Kampuni imepitia kipindi kigumu cha kusitishiwa huduma lakini wameishukuru LATRA kwa kuwapa nafasi nyingine ya kuzungumza na kuweza kupewa maelekezo.

“Tumepitia kipindi kigumu na tunaahidi kuzingatia yale ambayo ni mapungufu katika masharti ya leseni ya usafirishaji na tutaenda kuyafanyia kazi na tunaamni tutakuwa watu bora katika utoaji huduma ya usafirishaji” amesema Njoka.




*Bw. Salum Pazzy, Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano na LATRA (wa katikati) akizungumza na vyombo vya habari Septemba 20, 2024 ofisi za LATRA Mkoa wa Dar es Salaam kuhusu kurejesha huduma za Leseni kwa Mabasi sita ya kampuni ya Katarama Luxury.*

# MAFANIKIO YA LATRA KATIKA KUTEKELEZA MAJUKUMU YAKE




*Mhe. Daniel Baran Sillo Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani akikabidhi Tuzo kwa ABC UPPER CLASS LTD ya mshindi wa tatu katika kundi la wasafirishaji wakubwa wenye mabasi zaidi ya 30 katika hafla ya uzinduzi wa wiki ya Nenda kwa Usalama Barabarani iliyofanyika uwanja wa Jamhuri jijini Dodoma Agosti 26, 2024.*

Sekta ya usafirishaji inachangia maendeleo na ukuaji wa uchumi kwa kasi na kwa kutambua umuhimu wa kuchochea zaidi maendeleo ya nchi, mwaka 2019, Serikali ilianzisha Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) kwa Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini Sura ya 413 kwa lengo la kudhibiti huduma za usafiri ardhini kwa njia ya Barabara, Reli na usafiri wa Waya. Mamlaka ilianza rasmi kutekeleza majukumu yake tarehe 29 Aprili, 2019 baada ya Sheria yake kutangazwa kwenye Gazeti la Serikal Na. 358 la tarehe 26 Aprili, 2019.

Tangu kuanzishwa kwa Mamlaka hii, imefanikiwa kutekeleza masuala mengi ambayo yameleta mabadiliko chanya ikiwa ni pamoja na kupunguza kadhia ambazo wananchi walikuwa wakizipata wanapotumia huduma za usafiri wa umma. Mafanikio ya LATRA yamechagizwa na uongozi mahiri wa Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Wizara ya Uchukuzi ambapo Mhe. Rais ameweka mazingira wezeshi ya uwekezaji na ubunifu wa hali ya juu katika udhibiti wa usafiri, hali inayochangia kwa kiasi kikubwa kuongeza uwekezaji na kuwezesha mitaji kuwa endelevu kwa wasafirishaji

Pia, Wizara ya Uchukuzi chini ya uongozi wa Mhe. Prof. Makame Mbarawa (Mb), Waziri wa Uchukuzi akisaidiwa na Mhe. David Kihenzile, Naibu Waziri wa Uchukuzi, Prof. Godius Kahyarara, Katibu Mkuu Wizara ya Uchukuzi na Bw. Ludovick Nduhiye, Naibu Katibu Mkuu, Wizara ya Uchukuzi wamefanya jitihada za makusudi kuhakikisha Mamlaka inatekeleza majukumu yake kwa kusimamia vizuri sekta ya usafirishaji nchini na wadau kupata huduma bora, na katika kipindi cha kuanzia mwaka 2019 ambapo LATRA ilianzishwa hadi sasa, Mamlaka imepata mafanikio makubwa kupitia utekelezaji wa majukumu yake ya kila siku.

> **"Mafanikio ya LATRA yamechagizwa na uongozi mahiri wa Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**
>
> *CPA HABIBU SULUO*

>>>**Inaendelea Uk. 35**

>>>Inatoka Uk. 34

# Matumizi ya Tiketi Mtandao


CPA Habibu Suluo, Mkurugenzi Mkuu wa LATRA anasema kuwa, miongoni mwa mafanikio yaliyopatikana ni kuboresha usafiri wa mabasi yaendayo mikoani kwa kuanzisha matumizi ya tiketi za kielektroni, maarufu kama Tiketi Mtandao.

CPA Suluo anasema, Mamlaka imeboresha huduma ya utoaji wa Tiketi Mtandao ambao umepunguza ulanguzi wa nauli uliokuwa unafanywa na baadhi ya wasafirishaji wenye tamaa ya kujipatia faida kwa kuumiza abiria na kutokuwa na nia njema kwa maendeleo ya watu wengine na nchi yetu. Hii imewezekana kwa kuwa ndani ya mfumo wa Tiketi Mtandao, nauli zilizowekwa ni zile zilizoidhinishwa na Serikali kupitia LATRA na hivyo mwananchi anayesafiri hulipa nauli halali.

Uanzishwaji wa mfumo huu, ulilenga kulinda mitaji, kudhibiti ukusanyaji wa mapato na kuwaongezea wamiliki mapato, hivyo kuwa na mitaji endelevu na kupata faida kwa biashara ya usafirishaji wanayoifanya. Mfumo huu unasaidia kuhifadhi kumbukumbu na taarifa za abiria na kuwasilisha madai ya fidia endapo kutajitokeza changamoto yoyote katika safari zao.

## Utengenezaji wa Kanuni za Usafiri Ardhini na Ushirikishwaji wa Wadau

CPA Suluo anasema Serikali kupitia LATRA imeboresha na kutengeneza Kanuni mpya zinazoboresha sekta ya usafiri ardhini ambapo mchakato wake ulishirikisha Wadau wa ndani na nje ya Mamlaka, Taasisi za Serikali, Asasi Binafsi na wadau wengine wanaohusika. Kanuni mpya sita (6) zilizoandaliwa chini ya Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini, Sura ya 413 zimetangazwa Januari 12, 2024 katika Gazeti la Serikali Na. ISSN 0856-0323.




>>>Inaendelea Uk. 36



*CPA Habibu Suluo, Mkurugenzi Mkuu Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA), akimfahamisha jambo Dkt. John Mahona Makamu Mkuu wa Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT) kwenye Maonesho ya wiki ya Nenda kwa Usalama Barabarani Uliofanyika uwanja wa Jamhuri jijini Dodoma Agosti 26, 2024.*

>>>**Inatoka Uk. 35**

# Safari za Mabasi kwa Saa 24

Aidha, CPA Suluo anasema, Serikali inasisitiza suala la ushirikishwaji wa wadau, hasa wa sekta binafsi, kwani wao ndio walipa kodi na wana mchango mkubwa katika kujenga uchumi wa nchi yetu. Mamlaka inawashirikisha wadau wake katika hatua zote muhimu kabla ya kufanya uamuzi katika masuala yanayowahusu. Wadau hao wamekuwa wakishiriki katika vikao na mikutano inayolenga kusikiliza changamoto na kero mbalimbali ili kuzitafutia ufumbuzi kwa pamoja, pia kupokea mrejesho, maoni, mapendekezo na ushauri kabla ya kutoa uamuzi.

CPA Suluo anasema Safari za saa 24 kwa mabasi ya abiria zilisitishwa na Serikali miaka ya 1990 kwa sababu mbalimbali hususan za kiusalama na wananchi walikuwa na kiu ya kuona safari hizi zinarejea. Serikali ilizingatia maoni ya wadau wote muhimu, hali ya usalama barabarani, ubora wa miundombinu na maendeleo ya teknolojia ya habari kisha ikaridhia kuzirejesha. LATRA ilishiriki katika maandalizi ya kuruhusu mabasi kusafiri usiku baada ya Tamko la Serikali ambapo safari zilirejea rasmi tarehe 1 Oktoba, 2023 baada ya Mhe. Jumanne A. Sagini (Mb), aliyekuwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi na Mwenyekiti wa Baraza la Taifa la Usalama Barabarani kutoa Taarifa kwa Umma tarehe 29 Septemba, 2023.

Hakika jambo hili liliibua hisia za furaha kwa wananchi na wadau mbalimbali wa sekta ya usafiri ardhini nchini ambapo Serikali kwa kukata kiu ya wananchi hatimaye safari za usiku zikaanza na zimesaidia kukuza shughuli za kijamii na kiuchumi kwa mtu mmoja mmoja, wasafirishaji na Serikali kwa jumla na LATRA imeweka utaratibu maalumu ikiwa ni pamoja na masharti ya ziada kwa wasafirishaji wanao omba ratiba hizo. Hii ni pamoja na masharti ya kuwepo ithibati kwa madereva wa usiku kutumia Kitufe cha Utambuzi (i-Button) ili kurahisisha ufuatiliaji na kudhibiti ratiba za madereva kupumzika baada ya kuendesha kwa saa nane.

>>>**Inaendelea Uk. 37**

# Kuongezeka kwa Mapato ya Mamlaka

>>>Inatoka Uk. 36

CPA Suluo anasema mapato ya Mamlaka yanaongezeka kila mwaka na kwa mwaka wa fedha 2021/22 hadi 2022/23, mapato ya Mamlaka yaliongezeka kutoka Shilingi Bilioni 28.82 hadi Shilingi Bilioni 34.80 ikiwa ni ongezeko la Shilingi Bilioni 5.98 sawa na ongezeko la 20.7%. Aidha, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2022/23 hadi 2023/24, mapato ya Mamlaka yaliongezeka kutoka Shilingi Bilioni 34.80 hadi Shilingi Bilioni 35.92 (kabla ya kukamilika ukaguzi wa CAG) ikiwa ni ongezeko la Shilingi Bilioni 1.12, sawa na ongezeko la 3.2%.

Kwa mwaka wa fedha 2021/22 hadi 2023/24, mapato ya Mamlaka yaliongezeka kutoka Shilingi Bilioni 28.82 hadi Shilingi Bilioni 35.92 (kabla ya kukaguliwa na CAG) ikiwa ni ongezeko la Shilingi Bilioni 7.10 sawa na ongezeko la 24.6%.

## Kuchangia Mfuko Mkuu wa Serikali

CPA Suluo anasema, kipindi cha mwaka wa fedha 2022/23 hadi 2023/24 Mamlaka imeweza kuchangia Shilingi Bilioni 13.50 katika Mfuko Mkuu wa Serikali. Ameeleza pia kuwa, Mamlaka imeweza kuchangia taasisi mbalimbali za kitaifa na kimataifa kwa niaba ya Serikali ikiwa ni sehemu ya matumizi yake. Taasisi hizo ni pamoja na Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Usafiri Ardhini (LATRA CCC), Tume ya Ushindani (FCC), Baraza la Ushindani Tanzania (FCT), Jukwaa la Afrika la Wadhibiti wa Huduma (African Forum for Utilities Regulators - AFUR) na Umoja wa Taasisi za Reli Kusini mwa Afrika (Southern Africa Railways Association - SARA).

## Ukaguzi wa Hesabu za Mamlaka

CPA Suluo anafafanua kuwa, katika kipindi cha miaka yote tangu kuanzishwa kwa Mamlaka, LATRA imekuwa ikipata **HATI SAFI (Clean Audit Report)** kutoka kwa Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali (CAG) na kwa mwaka 2023/24, taarifa ya CAG inasubiriwa na matarajio ni kuendelea kupata hati safi.

>>>Inaendelea Uk. 38



# Mfumo wa kufuatilia Mwendo wa magari (VTS)

>>>Inatoka Uk. 37



Bw. Johansen Kahatano, Mkurugenzi wa Udhibiti Usafiri wa Barabara - LATRA anasema, tangu kuanzishwa kwa mfumo wa VTS mwaka 2017, Mamlaka imefanikiwa Kuunganisha jumla ya magari 11,154 kwenye mfumo huu ambapo, magari 8,265 yanaonekana yakiendelea kutoa taarifa (yapo hai) na 2,889 hayatumi taarifa kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo kufanyiwa kwa matengenezo na zinazo pata ajali barabarani. VTS imesaidia kupunguza madhara ya ajali zinazotokana na mwendokasi, Kurahisisha uchunguzi wa ajali pale zinapotokea, pamoja na Kumtambua dereva anayeendesha gari kupitia kitufe cha utambuzi (i-Button) ambacho kinaunganishwa moja kwa moja na mfumo wa VTS.

Vilevile Mfumo huu umeunganishwa kwenye vichwa 18 vya treni ambapo vichwa viwili (2) ni vya treni ya Shirika la Reli Tanzania (TRC) na vichwa 16 ni vya Mamlaka ya Reli ya Tanzania na Zambia (TAZARA).

## Utoaji wa leseni za usafirishaji

Aidha, katika kipindi cha mwaka 2022/23 hadi 2023/24, idadi ya leseni za usafirishaji zilizotolewa kila mwaka ziliongezeka kutoka 284,158 hadi 326,576 sawa na ongezeko la leseni 42,418 ambalo ni ongezeko la asilimia 15. Pia, ikilinganishwa na Mpango wa Mwaka 2023/24, LATRA ilipata mafanikio makubwa ya kuvuka malengo kwenye utoaji wa leseni za usafirishaji wa abiria na mizigo.

Anaongeza kuwa, LATRA imesaini Hati ya Maelewano (MoU) na Halmashauri (LGAs) 120 kati ya 185 Nchini kwa lengo la kukasimu LGAs jukumu la kutoa leseni za pikipiki za magurudumu mawili na pikipiki za magurudumu matatu (Bodaboda na Bajaji ) kwa niaba ya LATRA. Katika kipindi cha miaka mitatu (3), LATRA ilirejesha kwa halmashauri mbalimbali nchini, gawio la ada za leseni zilizofikia jumla ya Shilingi 1,787,543,180 (2020/21-Shilingi 297,404,000; na 2021/22-Shilingi 411,513,000 na 2022/23 - Shilingi 506,004,000 na 2023/24; Shilingi 572,622,180.

Vilevile, Mamlaka imeanzisha huduma mpya ya magari maalum ya kukodi (Special Hire) iliyoleta ahueni kwa wananchi ambapo kwa sasa wanayatumia kufanikisha shughuli zao za kijamii jambo ambalo kwa miaka ya zamani kabla ya huduma hii ilikuwa inaleta changamoto kwa wananchi.

>>>Inaendelea Uk. 39

# Uthibitishaji wa Madereva na Usajili wa Wahudumu

>>>Inatoka Uk. 38

Bw. Kahatano anasema, katika kutekeleza jukumu la kuwathibitisha madereva wa vyombo vya moto kibiashara kwa mujibu wa sheria, Mamlaka imekuwa ikiwasajili madereva na baadae kuwathibitisha. Serikali imefanya jitihada za makusudi za kupunguza ajali barabarani na kuiheshimisha tasnia ya udereva kwa kuiwezesha LATRA kutengeneza mfumo wa kielektroni wa kutahini madereva.

"Hadi kufikia tarehe 31 Septemba, 2024, zaidi ya madereva 26,538 wamesajiliwa na kuingiza taarifa zao kwenye kanzidata ya Mamlaka. Miongoni mwa madereva hawa, madereva 3,377 wamefaulu mitihani ya kuthibitishwa na LATRA na kati yao madereva 3,193 wamesajiliwa kwenye Mfumo wa Kufuatilia Mwenendo wa Magari (VTS) na kupatiwa kitufe maalumu cha utambulisho (i-Button) kinachowezesha utambuzi wa dereva anayeendesha gari kwa wakati husika kupitia mfumo VTS," amesema Kahatano.

Aidha, LATRA imetelekeza jukumu la kuwasajili wahudumu wa vyombo vya moto kibiashara ambapo hadi sasa Mamlaka imefanikiwa kusajili jumla ya wahudumu 279. LATRA kwa kushirikiana na taasisi nyingine kama vile Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT) na Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE); tarehe 1 Julai, 2023 ilifanya uzinduzi wa Mtaala ambao umeanza kutumika kufundishia wahudumu na mafunzo yalianza rasmi Oktoba 2023. Lengo ni kuhakikisha kuwa wahudumu wanafahamu Sheria, Kanuni na Taratibu za usafiri ardhini pamoja na kupata uelewa wa namna bora ya kuwahudumia wateja wao pindi wanapokuwa kwenye majukumu yao. LATRA, inapenda kuona wahudumu hawa wanakuwa nadhifu, wanaheshimu na kuheshimika

>>>Inaendelea Uk. 40



*Baadhi ya Madereva wa Vyombo vya Moto Kibiashara wakiwa katika chumba cha mtihani ofisi za LATRA Mkoa wa Dar es Salaam.*

# Udhibiti Usafiri wa Reli




>>>Inatoka Uk. 39

Mha. Hanya Mbawala ni Mkurugenzi Udhibiti Usafiri wa Reli kutoka LATRA, anasema anajivunia mafanikio makubwa ikiwemo uboreshaji wa miundombinu ya reli kwa Shirika la Reli Tanzania (TRC) na Mamlaka ya Reli Tanzania na Zambia (TAZARA) na hivyo kuendelea kurahisisha shughuli za wananchi kupitia reli.

Safari za Treni ya Reli ya Kisasa (SGR) ilizinduliwa rasmi Julai 25, 2024 na Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan Rais, wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, hii ni baada ya LATRA kufanya ukaguzi wa mabehewa na kuhakiki ubora wa mabehewa ya Reli ya Treni ya Kisasa (SGR) yaliyotengenezwa nchini Korea, na kutoa ithibati ya ubora kwa ajili ya TRC kutoa huduma kwa mabehewa hayo baada ya kujiridhisha ubora na usalama wa mabehewa na muindombinu.

Tathmini inaonesha kwamba, makosa ya kibinadamu katika uendeshaji wa shughuli za reli huchangia zaidi ya asilimia ya 85% ya ajali zote za treni kwa TRC na TAZARA. Mamlaka imeendelea kutoa semina kwa Wafanyakazi muhimu wa Usalama katika uendeshaji wa reli (Safety Critical Workers) kwa TAZARA na TRC ili kuwaongezea ujuzi wa kutimiza majukumu yao kwa weledi.

Pia anasema kuwa, LATRA itaendelea kufanya kaguzi mbalimbali kwenye miundombinu ya reli za Shirika la Reli Tanzania (TRC) na Mamlaka ya Reli Tanzania na Zambia (TAZARA) ili kubaini mapungufu yanayoweza kuhatarisha usalama.

> **"Mamlaka imeendelea kutoa semina kwa Wafanyakazi muhimu wa Usalama katika uendeshaji wa reli (Safety Critical Workers) kwa TAZARA na TRC ili kuwaongezea ujuzi wa kutimiza majukumu yao kwa weledi.**
>
> *MHA. HANYA MBAWALA*

>>>Inaendelea Uk. 41

## Udhibiti wa Usafiri wa Waya

>>>Inatoka Uk. 40

Bw. Abdallah Mhagama ni Mkurugenzi Udhibiti Uchumi LATRA ambaye anaeleza kuwa, usafiri wa Waya ni moja kati ya aina za usafiri mijini na maeneo yenye milima au kwenye vivuko ambao kwa sasa umeenea sehemu nyingi duniani na pia ni kivutio cha utalii. Utafiti wa awali umeonesha kuwepo fursa za uwezekano wa kuwekeza usafiri huu kitalii hapa nchini, ili kuunga mkono juhudi za Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ambaye yeye mwenyewe ameshiriki kutangaza fursa za utalii nchini kupitia filamu ya The Royal Tour. Maeneo yenye fursa hiyo ni Arusha, Kilimanjaro, Mbeya, Iringa, Morogoro, Tanga na Dar es Salaam, "tumeshaandaa rasimu ya Kanuni ya Udhibiti wa Usafiri wa Waya ambazo zinaendelea na hatua mbalimbali ili zitakapokamilika, zitapata idhini ya Waziri mwenye dhamana na zitasaidia kusimamia uwekezaji na utumiaji huduma hiyo kwa ufanisi."

## Udhibiti wa Viwango vya Nauli

Bw. Mhagama anasema, LATRA ina jukumu la kisheria la kudhibiti viwango vya tozo za huduma zinazodhibitiwa. Katika kutekeleza hili, Mamlaka ilifanya mapitio ya viwango vya nauli za mabasi ya masafa marefu, mabasi yanayotoa huduma ndani ya mji (daladala), ambazo zilitangazwa katika Gazeti la Serikali Toleo Na. 47 la tarehe 24 Novemba, 2024 na Mamlaka iliutangazia umma kuanza kutumia rasmi nauli hizo ifikapo Disemba 8, 2024

Pia, Amri ya Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini ya Nauli za Abiria kwa Daraja la Kawaida kwa Treni ya SGR Na. 01 ya Mwaka 2024 ilitangaza rasmi nauli za treni za abiria zinazotumia Reli ya Kisasa (Standard Gauge Railway - SGR) tarehe 14 Julai, 2024

>>>Inaendelea Uk. 42



# Matumizi ya TEHAMA

>>>Inatoka Uk. 41

Mha. Eliud Kataraihya ni Mkuu wa Kitengo cha TEHAMA LATRA ambaye anasema, mamlaka imeboresha mifumo inayotumia, ikiwemo Mfumo wa Usimamizi wa Shughuli za Kiudhibiti (RRIMS) unaotumika kwa ajili ya maombi ya leseni za usafirishaji pamoja na kazi zingine za usimamizi wa shughuli za kiudhibiti za Mamlaka. Mfumo huo umeunganishwa na mifumo ya taasisi nyingine za Serikali kama vile TRA, TIRA, NIDA, GePG na BRELA pamoja na mifumo ya wadau wengine kama vile watoa huduma wa Tiketi Mtandao. Lengo la kuunganisha ni kurahisisha utoaji huduma za Mamlaka kwa wananchi. Mfumo huu hutumika kutoa leseni za usafirishaji na unamuwezesha mteja kufanya maombi popote alipo na kuchapa leseni yake popote alipo bila kufika ofisi za LATRA.

Anaeleza kuwa, Maombi ya leseni yanayowasilishwa yanafanyiwa kazi siku hiyo hiyo na kuhakikisha mwananchi anapata leseni chini ya saa 24. Aidha, Mamlaka imeboresha mfumo huu na kuanza kutoa leseni za kielektroni na kuondoa hitaji la wateja kutembelea ofisi za Mamlaka kwa ajili ya kufuata leseni.

Vilevile anasema, Mamlaka imeboresha utoaji wa Huduma ya usafiri wa kukodi kwa njia ya mtandao ambayo imeendelea kukua kwa kasi kubwa tangu ilipoanza hapa nchini mwaka 2017. Hadi sasa, jumla ya Kampuni 22 zenye mifumo ya kutoa huduma ya teksi/pikipiki mtandao (ride hailing platform operators) ziliwasilisha maombi ya Leseni LATRA na yalikidhi mahitaji ya kisheria ambapo kampuni 22 zimeshalipia ada za leseni na kupatiwa leseni hizo. Pia, leseni ambazo zimetolewa kwa teksi/pikipiki mtandao hadi sasa ni 21,575 zenye uhai wa mwaka mmoja." amefafanua Mha. Kataraihya.

Aidha anasema, huduma hiyo inadhibiti mmiliki wa mfumo wa teksi/pikipiki mtandao, mmiliki (dereva) wa gari, na abiri (nauli). Hivyo, Mamlaka inapopanga nauli za huduma hiyo, inaweka kiwango cha chini (kisishuke) ili kumlinda mmiliki wa gari au dereva na kiwango cha juu (kisizidi) kumlinda abiria. **Mmiliki wa mfumo ya teksi/pikipiki mtandao yeye anapata kamisheni ya nauli, nayo kuna kima cha chini na cha juu) ambacho kinatoa uhuru kwa wamiliki (madereva) kumchagua mwenye nafuu na maslahi kwake.**

>>>Inaendelea Uk. 43



>>>Inatoka Uk. 42




Mamlaka imetengeneza Mfumo wa Taarifa kwa Abiria (Passenger Information System - PIS) unaopatikana kwa anwani ya https://pis.latra.go.tz/ kupitia simu janja au kompyuta na pia umefungwa katika runinga za stendi ya mabasi Magufuli Dar es Salaam na stendi ya mabasi Nanenane jijini Dodoma. PIS ni stendi kiganjani kwa mwananchi na imeboresha upatikanaji wa taarifa kwa abiria mbapo mwananchi anaweza kufahamu muda basi litawasili kituoni , kufahamu muda unaotarajia kufika kule aendako, kufahamu mwendokasi wa basi, kufahamu jina la mmiliki wa basi pamoja na kufuatilia basi likiwa safarini.

Rais Dkt Samia Suluhu Hassan amekuwa akisisitiza mifumo ya Serikali kuunganishwa na kubadilishana taarifa na kwa kuzingatia maelekezo haya, Mfumo wa PIS umetokana na Mfumo wa Kufuatilia Mwenendo wa Magari (VTS) ambapo limefunguliwa dirisha dogo litakalomwezesha mwananchi kupata taarifa za basi husika pindi awapo safarini au anapotaka kusafiri au anapomsubiri mgeni aliyepo ndani ya basi.

Pia, kuna mfumo tumizi wa LATRA (LATRA App) uliotengenezwa na Mamlaka na unapatikana 'Play Store' kwenye simu zote za Android unaomwezesha mwananchi kupata taarifa za nauli za mabasi ya masafa marefu na mabasi ya mijini (daladala) na kwa sasa Mamlaka inaendelea kuboresha huduma za mfumo huo na hivi karibuni inatarajia kuwezesha upatikanaji wa taarifa kuhusu dereva aliyesajiliwa na kuthibitishwa na LATRA kupitia Mfumo huu ikiwa ni sehemu ya maboresho pamoja na kuwezesha upatikanaji wa App hiyo kwa simu za iOS.

Mifumo mingine inayotumiwa na Mamlaka ni Mfumo wa e-Mrejesho unaotumika kwa ajili ya kupokea Malalamiko, Mapendekezo, Pongezi au Maulizo. Mfumo unapatikana kwa anwani ya https://emrejesho.gov.go.tz/ au kwa kupakua Mobile App ya eMrejesho au kwa kutumia simu yako kwa njia ya Msimbo (USSD) au kwa kupitia tovuti ya Mamlaka https://www.latra.go.tz/ sehemu ya tovuti mashuhuri. Pia Mfumo Jumuishi wa Huduma kwa Wateja unaopatikana kwa anwani ya https://callcenter.gov.go.tz/ pamoja na Mfumo wa Taifa wa Ununuzi wa Umma wa Kieletroni (NeST) ambapo Mamlaka imejiunga na inatumia kwa ajili ya kutangaza na kuchakata zabuni mbalimbali.

> **"Mfumo Jumuishi wa Huduma kwa Wateja unaopatikana kwa anwani ya https://callcenter.gov.go.tz/**
>
> *MHA. ELIUD KATARAIHYA*

>>>Inaendelea Uk. 44

>>>Inatoka Uk. 43

# Uboreshaji wa huduma za LATRA kupitia vyama vya ushirika

Mamlaka inaboresha huduma za usafiri zinazotolewa na wamiliki wa pikipiki za magurumu mawili (Bodaboda) pamoja na pikipiki za magurumu matatu (Bajaji) kwa kushirikiana na vyama vya ushirika vinavyofanya kazi ya utoaji leseni kwa niaba ya LATRA.

Johansen Kahatano, Mkurugenzi Udhibiti Usafiri wa Barabara anasema kuwa "Kufuatia uboreshaji wa huduma zitolewazo na bodaboda na bajaji, Mamlaka imeridhia zifanye kazi chini ya kivuli cha Vyama vya Akiba na Mikopo (SACCOS) na kupitia huu utaratibu tumekubaliana kuwapatia kazi ya kukata leseni kwa niaba ya Mamlaka na kwa kufanya hivyo, watapatiwa kamisheni kulingana na mapato watakayoyakusanya ili kuimarisha vyama vyao na kupata mtaji wa kutosha kujiendeleza shughuli zao za kiuchumi, kupitia hii tunawajengea uwezo wa kujisimamia wao wenyewe."

Aidha kupitia vyama vya ushirika, Mamlaka imefanikiwa kurejesha kiasi cha Shilingi 2,446,400/= kwa Chama cha Ushirika wa Akiba na Mikopo cha Bajaji na Bodaboda mkoani Kilimanjaro (KIBABOT SACCOS) ikiwa ni sehemu ya gawio la 20% ya leseni zilizotolewa na chama hicho kwa miezi mitano ya majaribio kwa niaba ya LATRA.

> **"Tumekubaliana kuwapatia kazi ya kukata leseni kwa niaba ya Mamlaka na watapatiwa kamisheni kulingana na mapato watakayoyakusanya ili kuimarisha vyama vyao**
>
> *Bw. Johansen Kahatano*

>>>Inaendelea Uk. 45



*Bw. Kiseo Yusuf Nzowa, Katibu Tawala Mkoa wa Kilimanjaro, aliyemuawakilisha Mgeni Rasmi Mhe. Nurdin Hassan Babu Mkuu wa Mkoa Kilimanjaro, akikabidhi cheti cha Uwakala wa kutoa Leseni za LATRA kwa Chama cha Ushirika Mikopo na Akiba cha Bajaji na Bodaboda mkoani Kilimanjaro (KIBABOT SACCOS) Septemba 03, 2024 katika Ukumbi wa Mikutano ofisi ya Mkuu wa Mkoa – Kilimanjaro.*

# Kuhamasisha ushindani wenye ufanisi miongoni mwa watoa huduma zinazodhibitiwa

>>>**Inatoka Uk. 45**

CPA Habibu Suluo, Mkurugenzi Mkuu LATRA, amesema Kifungu cha 6(a) cha Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini Sura ya 413, kimeipa LATRA wajibu wa kuhamasisha ushindani wenye ufanisi miongoni mwa watoa huduma zinazodhibitiwa.

Katika kutekeleza wajibu huo, Mamlaka iliendesha zoezi la ushindani kwa wasafirishaji wa mabasi ya masafa marefu kwa kuwashindanisha katika makundi matatu ambayo ni wasafirishaji wakubwa (wenye mabasi zaidi ya 30), wasafirishaji wa kati (wenye mabasi 11 hadi 30) na wasafirishaji wadogo (wenye mabasi 3 hadi 10).

Washindi walikabidhiwa tuzo zao na Mhe. Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, na Mhe. Daniel Baran Sillo, Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi na Mwenyekiti wa Baraza la Taifa la Usalama Barabarani, Agosti 26, 2024 katika sherehe za ufunguzi wa Maadhimisho ya Wiki ya Nenda kwa Usalama Barabarani yaliyofanyika kitaifa uwanja wa Jamhuri jijini Dodoma.

Aidha, tuzo hizo zimetolewa ili kuchochea utoaji wa huduma bora na salama ya usafirishaji wa abiria kwa ufanisi na ubunifu hususan katika matumizi sahihi ya teknolojia.

## Kuwafikia Wadau

LATRA imeendelea kuwafikia wadau wake kupitia vipindi vya elimu kwa umma vinavyorushwa kila siku ya Jumanne kupitia Chaneli ya Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC1) na Clouds TV pamoja na mitandao ya kijamii. Vilevile inashiriki katika maonesho mbalimbali ya Kitaifa na kimataifa, na kwa kutumia namba za bila malipo 0800110019 au 0800110020 zinazopatikana saa 24 siku saba za wiki ambapo wananchi wanawasiliana na Mamlaka na kutatua changamoto zao kwa wakati.

Pia, Serikali kupitia LATRA inaendelea kuboresha huduma za usafiri ardhini na kuhakikisha upatikanaji wa huduma hizo zinakuwa rahisi, zenye tija na manufaa kwa Serikali, Wananchi na Watoa Huduma kwa jumla.




*Wadau mbambali wakipatiwa elimu kuhusu kazi na majukumu yanayotekelezwa na Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) walipotembelea banda la LATRA kwenye maonesho ya Kilimo ya Kimataifa – Nanenane jijini Dodoma Agosti 04, 2024.*


EPUKA MATAPELI
HATUPOKEI FEDHA TASLIMU,
MALIPO YOTE YA LATRA
YAFANYIKE KUPITIA NAMBA YA
MALIPO YA SERIKALI
TUPIGIE BILA MALIPO 0800 11 00 19/20
EPUKA VISHOKA
HUDUMA ZA LATRA NI RAFIKI,
ZA WAZI NA ZINAPATIKANA
KWA MUDA MFUPI.
HATUPOKEI RUSHWA
USITOE RUSHWA KWA AJILI YA
KUPATA HUDUMA ZA LATRA
UKIBAINI VITENDO VYA RUSHWA
TUPIGIE BILA MALIPO
0800 11 00 19/20

# Usafiri Ardhini

Jarida hili limeandaliwa na Kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano cha Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA), likiongozwa na Bodi ya Wahariri

**Mwenyekiti:** CPA HABIBU SULUO | **Mhariri Mkuu:** SAMUEL KEENJA | **Wahariri Wasaidizi:** SALUM PAZZY, MAMBWANA JUMBE | **Waandishi:** MAMBWANA JUMBE, NANCY AMANI na MARIAM NINA | **Msanifu Jarida:** IBRAHIM SAID



***Pamoja kwa Usafiri Bora***